# Nipashe

Jumatano Juni 19, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581712

www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



UK. 21

**MBAPPE AEPUKA UPASUAJI WA PUA**

**RAS** afa ajalini kumlaki Mpango, watumishi Afya nao wafia njiani wakienda kula Sikukuu ya Idd



UKURASA 3 & 5

**RIPOTI MAALUM -3**

Wafanyakazi wa kiwanda cha UFI wasotea stahiki zao miaka 26

UKURASA 4



**Tanzania** kujenga maghorofa pacha ubalozini Nairobi

UKURASA 19

# Mwanga mpya

• **Samia** atoa miezi sita serikali imalize kulipa madeni ya vyombo vya habari; amwagia sifa Mhariri Mtendaji Nipashe... *ukurasa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan akipokea Ripoti ya Kamati Maalum ya Kutathmini Hali ya Utendaji na Uchumi wa Vyombo vya Habari Tanzania Bara kutoka kwa Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mwandishi Mbobevu Tido Mhando wakati wa Kongamano la Pili la Maendeleo ya Sekta ya Habari, Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## YALIYOMO

**UKURASA WA 17**

**'UPATIKANAJI MAWASILIANO YA UHAKIKA BADO TATIZO Z'BAR'**



SPIKA wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Zuberi Ali Maulid, amesema bado kuna changamoto ya upatikanaji wa huduma ya mawasiliano ya uhakika kwa baadhi....

**UKURASA WA 24**

**SAIDO ASEPA NA MABAO 24 SIMBA**



KLABU ya Simba imeachana na kiungo mshambuliaji wake tegemeo, Saido Ntibazonkiza, baada ya kuhudumu kwa msimu mmoja na nusu, akipachika jumla ya mabao 24 katika mechi za Ligi Kuu Tanzania...

## Spika Tulia ampeleka Mpina Kamati ya Maadili

UKURASA 19



## Mtoto mwenye ualbino akutwa bila viungo, Rais Samia aingilia kati

UKURASA 3

**MICHEZO** **MSUVA AFUNGUA MILANGO YANGA** UK.24 **MAONI,** UK.6

# Mwanga mpya vyombo vya habari

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan ametoa miezi sita kwa wizara na taasisi za umma zinazodaiwa na vyombo vya habari kuhakiki madeni na kukaa pamoja kujadili watakavyoyalipa.

Amewakumbusha waandishi kuandika habari zenye kuleta mawazo kinzani ya kujenga nchi badala ya kuchochea migogoro na mipasuko ya kutishia amani ya nchi.

Pia, aliwapongeza waandishi mbalimbali waliopata tuzo za kimataifa kwa kuiwakilisha Tanzania na kuiletea sifa, akiwamo Mhariri Mtendaji wa Nipashe, Beatrice Bandawe, aliyetunukiwa tuzo ya mwanamke kiongozi kwenye chumba cha habari Afrika, inayotolewa na Umoja wa Wachapishaji Duniani (WAN IFRA) akiwa ni Mtanzania wa kwanza.

Wengine ni Mhariri Mtendaji gazeti la Jamhuri, Deodatus Balile, aliyechaguliwa kuwa Rais wa Jumuiya ya Wahariri Mashariki mwa Afrika, Ernest Sungura, Mwenyekiti wa kwanza Mtandao wa Mabaraza Huru barani Afrika na Kajubi Mukajanga kuwa kiongozi wa Baraza la Vyombo vya Habari Afrika Mashariki.

Rais Samia aliyasema hayo jana wakati akihutubia Kongamano la pili la Maendeleo ya Sekta ya Habari nchini lililofanyika jijini Dar es Salaam.

Akizungumzia madeni ya vyombo vya habari, aliahidi serikali itayalipa ifikapo Desemba, mwaka huu.

Alisema ataiagiza Wizara ya Fedha kufanya uhakiki wa madeni ya serikali ili yanayolipika yalipwe huku akiahidi kusimamia suala hilo.

Aliwakumbusha wamiliki wa vyombo vya habari wakati serikali inawalipa madeni hayo, wawalipe wafanyakazi wao mishahara yao. Alisema kutowalipa kunapunguza ari ya kufanya kazi na kudhorotosha maendeleo ya sekta ya habari.

Aliwashangaa waandishi wa habari kuwa hodari kuandika mambo ya watu wengine wakati wao wanakabiliwa na changamoto nyingi ikiwamo kutolipwa mishahara na waajiri wao na hawasemi chochote.

Kadhalika, alisema sasa ni wakati wa vyombo vya habari kujiendesha kibiashara ili kuepuka madeni yasiyolipika yanaonekana kuwa mengi na kuchangia kwa kiasi kikubwa kuwatia hasara.

Akizungumzia mabadiliko ya teknolojia, alisisitiza umuhimu wa kufikiria kuwekeza kwenye habari za mtandaoni kwa kuwa wasomaji wa magazeti ya kuchapisha wamepungua na pia malighafi za kuchapishia zimepungua kutokana na wazalishaji wakuu ambao ni nchi ya Ukraine kuathirika na vita, hali inayochangia kudorora kwa biashara zao.

### UWAJIBIKAJI

Rais Samia alisema, amefanya juhudi kuimarisha uhuru wa vyombo vya habari na kusisitiza ni wajibu wao kuutumia kwa weledi na kuzingatia dhana ya uwajibikaji kwa sababu vina kazi muhimu ya kuunganisha serikali na wananchi na kuleta mabadiliko chanya katika jamii.



Rais Samia Suluhu Hassan akifungua Kongamano la Pili la Sekta ya Habari jana. **PICHA: MTANDAO**

Kuelekea katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu mwakani, alisema kalamu za waandishi wa habari zinahitajika kwa ajili ya kujenga na si kubomoa kwa kuleta migongano ya kisiasa.

"Kwa maneno mengine msitoboe dau tunalosafiria, ndani ya hilo dau tupo wote, ukitoboa yakiingia maji tunazama wote, msiingie kwenye mtego wa kurarua nyuzi zinazounganisha kitambaa cha taifa letu," alisema.

Alisema uhuru wa vyombo vya habari haumaanishi kutoa lugha ya matusi, kashfa wala kejeli bali kutoa mawazo kinzani yenye lengo la kuboresha na kuijenga nchi ili kuleta maendeleo.

Alivitaka vyombo hivyo kuendana na kasi ya mabadiliko ya teknolojia huku vikijua wajibu wao wa kulinda mila, desturi na utamaduni na usalama wa kisiasa wa taifa hilo na si kuyahamasisha kwa kisingizio cha biashara.

Aliwakumbusha kutumia kalamu zao kuandika mambo yanayojenga nchi kwa kuwa yakiandikwa mambo mabaya yakasomwa nje ya nchi sifa ya nchi nzima inaharibika na si ya mtu mmoja.

Alisema kongamano hilo litumike kujitathmini ni wapi wanafanya vyema na wapi hawafanyi vizuri na kupanga mikakati ya namna ya kujiboresha kwa manufaa ya vyombo vyao na nchi kwa ujumla.

### ASISITIZA UCHAMBUZI

Amesisitiza vyombo vya habari kufanya uchambuzi wa kina taarifa wanazozipokea kabla ya kuziandika kwa kuwa nyingi zimekuwa zikiandikwa kama zilivyo na wakati mwingine kuleta taharuki.

Aidha, kuandika habari zinazokubalika na jamii badala ya kupata umaarufu na matokeo yake kuharibu hadhi ya mwandishi na chombo cha habari.

Alisema kuna baadhi ya waandishi wanachukua habari zilizoandikwa na mataifa mengine kuhusu nchi hiyo na kuziandika kama zilivyo bila ya kuzifanyia uchambuzi na kuwasihi kuwa wafafanuzi wa hoja kwa ajili ya kulinda hadhi zao wenyewe na nchi yao.

### HATUSHINDANI

Alisema vyombo vya habari si mshindani wa serikali bali ni mdau na mshiriki muhimu wa shughuli za serikali na kuuhabarisha umma masuala ya nchi yanayochochea maendeleo.

"Huko nyuma kipindi fulani vyombo vya habari na serikali vilikuwa vinavutana, wao wamevuta na sisi tumevuta, lakini tuliona hatutofika pahali pazuri hivyo tuliamua kukaa sehemu moja, kuzungumza na kufanya kazi kwa pamoja," alisema.

Alisema serikali haina budi kuweka mifumo ya kisera, kisheria na taasisi inayolenga kuimarisha uhuru wa mazingira kwa waandishi wa habari.

Alivishukuru vyombo hivyo kwa jinsi vinavyoshirikiana na serikali kutoa habari kwa umma kuhusu mambo yanayoendelea kwenye jamii ikiwamo harakati za maendeleo na hata majanga kama vile maporomoko ya Hanang' na athari za mvua za El-nino zilitokea miezi michache iliyopita.

### HABARI ZA VIJIJINI

Alisisitiza habari za vijijini ziripotiwe na vyombo vya habari vya jamii, wananchi wa maeneo hayo wapate kuzisikia, kwa kuwa taarifa nyingi zinaandikwa na vyombo vya kitaifa kama vile ITV, TBC, UTV.

Aliwaagiza wadau wa habari kuipelekea serikali mapendekezo ya kuundwa kwa mkakati wa mawasiliano nchini ili kuboresha sekta hiyo.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, alisema maboresho makubwa aliyoyafanya Rais Samia yameipandisha nchi chati kimataifa katika kuimarisha uhuru wa habari.

Alisema hilo limethibitishwa na Ripoti ya World Press Freedom Index ya mwaka 2024 inayoonyesha kuwa Tanzania imeongoza kwa nchi za Afrika Mashariki na duniani kushika nafasi ya 97 kutoka 143.

Alisema pia sifa hiyo imechochewa pia na mabadiliko ya mtanzamo wa waandishi wa habari kutokana na uzalendo mkubwa baina yao kwa kuwa katika utoaji taarifa zinazohusu nchi hiyo wametanguliza maslahi ya nchi.

Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo Zanzibar, Tabia Maulid Mwita, alisema wizara hiyo imekamilisha Sera ya Habari na wanatarajia kuizindua.

Alimshuruku Waziri Nape kwa kuwasaidia kuwapa wataalamu wengi ili kuhakikisha sheria hiyo inakuwa na maudhui sawa na Sheria ya Habari ya Tanzania Bara kwa kuwa wote wanatoka katika nchi moja.

Mwenyekiti wa Umoja wa Haki ya Kupata Taarifa (CoRi), Ernest Sungura aliiomba serikali kuondoa ukomo wa uwekezaji wasiokuwa wa Tanzania kumiliki hisa na kuwaruhusu wamiliki zaidi ya asilimia 49 ili kuchochea maendeleo ya sekta hiyo.

Alitaja changamoto zinazowakabili waandishi wa habari kuwa ni kufanya kazi bila mikataba na takwimu zikionyesha kuwa ni asilimia 80 wanaishi katika hali hiyo tofauti na Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini ya mwaka 2004.

Aidha, aliiomba serikali kupanua uhuru wa vyombo vya habari nchini ili kumpa uhuru kila mwandishi wa kutoa maudhui huku wakiimarisha misingi kusimamia maadili ya weledi katika kazi.

Akisoma Taarifa ya Hali ya Waandishi wa Habari, Utendaji na Uchumi wa Vyombo vya Habari nchini, Mwenyekiti wa kamati hiyo, Tido Muhando, aliainisha mambo waliyoyaona kuwa ni changamoto katika vyombo vya habari ikiwamo kuidai serikali na sekta binafsi madeni makubwa na ya muda mrefu.

Alisema hali hiyo imesababisha vyombo hivyo kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa wakati ikiwamo kuwalipa wafanyakazi mishahara na kulipa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT).

Aidha, alisema kutokana na hofu ya usalama wao, waandishi wa habari wameacha kuandika maudhui yanayolenga uwajibikaji na kudhoofisha waandishi kuzingatia uwajibikaji wa umma na kuwa na kizazi kisichofikiria sawa sawa, wengi wamebobea kwenye habari za burudani, vichekesho.

Kamati hiyo ilipendekeza pamoja na mambo mengine kuboreshwa kwa sera ya habari ili kuruhusu wawekezaji wa nje kumiliki hisa kwa asilimia 75, kwa sasa sera hiyo inaonyesha wawekezaji hao wanaweza kuwekeza chini ya asilimia 50.

Ilipendekeza kuwapo na mfuko wa mafunzo kwa vyombo vya habari yatakayowezesha kuletwa kwa kampuni za nje za teknolojia kwa ajili ya mafunzo pamoja akili bandia itumike katika vyombo vya habari.


## NOTISI/ TANGAZO LA GAZETI

**HEDANE ENTERPRISES (T) LIMITED** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya **MWANGA HAKIKA BANK LTD,** tunatoa notisi ya kulipa madeni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tangazo hili,vinginevyo tutafanya minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| NA. | JINA LA MDAIWA | JINA LA MWENYE DHAMANA | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | BENSON AUDAX CHAMLESILE | BENSON AUDAX CHAMLESILE | LANDED PROPERTY TITLE NO.118 153 PLOT NO.81 BLOCK NO," CE" | MAPINDUZI SNE, DODOMA | 05/07/2024 SAA 4 KAMILI NA KUENDELEA |
| 2 | BENSON AUDAX CHAMLESILE | BENSON AUDAX CHAMLESILE | LANDED PROPERTY EQUITABLE MORTGAGE(SALE AGREEMENT | MAPINDUZI SNE, DODOMA | 05/07/2024 SAA 6 KAMILI NA KUENDELEA |

**Vigezo na masharti ya mnada**

1. Ukaguzi wa dhamana unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Mali/dhamana itauzwa katika hali ilivyo na mahali ilipo.
3. Mshindi wa mnada at lazimika kulipa malipo yasiyo pungua 25% ya bei iliyofikiwa siku ya mnada, na 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha hatimiliki (transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenye nyumba/eneo lililouzwana bank (eviction) niza mnunuzi.
5. Mnunuzia akishindwa kutimiza sharti mojawapo hapo juu malipo ya awali hayatarejeshwa na mnada utarudiwa.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na:**

**Hedane Enterprises (T) Limited**
**City Centre Bulding**
**P. O. Box 1211, Arusha – Tanzania**
**Tel: +255 735 277 331/0759 648 448**
**Email: philbertmussali@gmail.com**
**hedaneenterprises@gmail.com**

HABARI KITAIFA

# Mwili wa mwenye ualbino wakutwa bila viungo, Rais Samia aingilia kati

## •RAS afa akiwahi kumlaki Mpango

**Na Waandishi Wetu**

VILIO vimetawala wakati mwili wa mtoto mwenye ualbino, Asimwe Novath (2) ukiopolewa baada ya kukutwa kwenye karavati, huku baadhi ya viungo vikiwa vimenyofolewa.

Mtoto huyo alichukuliwa mikononi mwa mama yake Mei 20, mwaka huu na watu wasiojulikana. Mwili umegundulika baada ya siku 19.

Juzi wananchi walishuhudia mwili ukiopolewa ukiwa umefungwa katika mfuko wa sandarusi, huku Kaimu Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Kagera, Yusuph Daniel, akithibitisha jeshi hilo kuwashikilia wanaume wanne kwa tuhuma za kuhusika na tukio hilo la kikatili.

Kutokana na tukio hilo, Chama cha Watu Wenye Ualbino Tanzania (TAS) kimeomba kuteta na uongozi wa juu serikalini, kikihofia usalama wa kundi hilo katika mchakato wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka huu na Uchaguzi Mkuu mwakani.

Mei 20, mwaka huu, mtoto huyo, mkazi wa Kijiji cha Bulamula, Kata ya Kamachumu, wilayani Muleba, mkoani Kagera, alichukuliwa mikononi mwa mama yake na watu wasiojulikana.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Muleba, Benjamin Mwikasyege, akizungumza na waandishi wa habari akiwa eneo ulikopatikana mwili huo, alisema ulikutwa chini ya daraja, ukiwa umefungwa kwenye mfuko wa sandarusi, huku baadhi ya viungo vikiwa vimenyofolewa.

"Mwili umekutwa chini ya daraja (lililoko barabara ya Makongora, Kitongoji cha Kabyonda, Kijiji cha Balele, Kata ya Ruhanga) kwenye karavati ukiwa umefungwa kwenye mfuko wa sandarusi. Kuna maji kidogo na kuna mfereji.

"Sote tunalaani tukio hili hasa kumpoteza mtoto huyu mwenye ualbino, kuna baadhi ya viungo ambavyo vimetolewa. Mwili huo umewekwa na watu ambao hawajafahamika. Baada ya kuufungua, viongozi wameendelea kuukagua," alisema Mwikasyege.

Alisema kuwa kupitia Jeshi la Polisi wataendelea na taratibu zao za kiuchunguzi, akisisitiza kuwa wote waliohusika, watakamatwa na kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

Kuua kwa kukusudia si tu kwamba ni kosa la jinai lenye adhabu ya hukumu ya kifo mahakamani, bali pia ni ukiukwaji wa Katiba ya Nchi, Ibara ya 14 inayoelekeza "Kila mtu anayo haki ya kuishi na kupata kutoka kwa jamii hifadhi ya maisha yake, kwa mujibu wa sheria."

**KAULI YA TAS**

Kaimu Katibu Mkuu wa TAS, Abdillah Omary, akizungumzia tukio hilo jana, alisema matarajio yao yalikuwa kumpata mtoto huyo akiwa hai, lakini kilichotokea kimewashtua.

Alisema wanahitaji kuonana na mamlaka kubwa ndani ya nchi ili kusaidia usalama wa kundi hilo, ikizingatiwa mwaka huu kuna Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu mwakani. Kumekuwa na matukio ya ukatili dhidi ya kundi hilo wakati wa mchakato wa uchaguzi nchini.

"Kama mwenye ualbino na mzazi mwenye watoto, ninajaribu kuwaza kwa siku zote ambazo mtoto huyo alichukuliwa mikononi mwa mama yake, alikuwa katika hali gani, wakati anafanyiwa madhira hayo yote alipitia hatua gani za uchungu," alisema.

Omary alikumbusha jamii kwamba ualbino hauwezi kufutwa nchini. Wanaodhani kundi hilo litawapa utajiri waondokane na fikra hizo na kila mmoja awe na wajibu kuhakikisha ulinzi na usalama kwao.

Alisema kuwa mwaka 2023, matukio yaliyojitokeza yalihusu ufukuaji makaburi na vitisho kwa kundi hilo na kwa mwaka huu, tayari kuna matukio mawili, likiwamo la kijana kujeruhiwa na wasiojulikana wakati akicheza nyumbani kwao.

Jana bungeni, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Khadija Taya, maarufu Keysha, aliomba mwongozo wa Spika, akitaka lijadili usalama wa wenye ualbino wakati wa mchakato wa uchaguzi.

Hata hivyo, Naibu Spika wa Bunge, Mussa Zungu, alisema mbunge huyo alikosea kanuni wakati wa kuwasilisha hoja yake na kumwelekeza kuonana na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ili amweleze vizuri kuhusu suala hilo.

Kaimu Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Kagera, Yusuph Daniel, aliiambia Nipashe jana kuwa hadi sasa wanashikilia wanaume wanne kutokana na tukio la Mei 20 mwaka huu, mwili wa mtoto huyo unasubiri ndugu zake ili taratibu za maziko zifanyike. Gharama zinabebwa na serikali.

Rais Samia Suluhu Hassan alisema jana kuwa kifo hicho cha mtoto mdogo mwenye ualbino kimemgusa, akitaka washiriki wa Kongamano la Sekta ya Habari kusimama kwa muda na kuomba kwa ajili ya kundi hilo.

**RAS AFA AJALINI**

Mkoani Kilimanjaro, ajali ya barabarani imekatisha uhai wa Katibu Tawala wa Mkoa huo, Dk. Tixon Nzunda, aliyekuwa akiwahi Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA), kumpokea Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango na ujumbe wake.

Dk. Nzunda na dereva wake walipoteza maisha jana alasiri baada ya gari lake aina ya VXR kugongana uso kwa uso na lori la kubeba nishati ya gesi safi, mali ya Kampuni ya Orange Gas, lenye namba za usajili T 655 ABY, aina ya Scania lililokuwa likitokea Arusha kwenda Moshi.

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, akitangaza kifo cha Dk. Nzunda, akisema Katibu Tawala huyo na dereva wake walipoteza maisha saa 8:30 mchana katika eneo la Mjohoroni (Palestina), wilayani Hai.

***Imeandaliwa na Romana Mallya na Godfrey Mushi.**


## Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya **epaper.ippmedia.com** utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza **"subscribe"**
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa **kadi ya benki** malipo kwa **mtandao wa simu** unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa **namba ya simu** unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. **Kwa benki** unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

6. Unafungua website yako ya **www.ippmedia.com** upande wa kulia utaona **"E-Paper"** utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

RIPOTI MAALUM -3

# Wafanyakazi wa kiwanda cha UFI wasotea stahiki zao kwa miaka 26



**Na Mwandishi Wetu**

**HII ni sehemu ya tatu ya ripoti inayoangazia kiwanda cha UFI (Ubungo Farm Implements) kilichoko Shekilango, wilayani Ubungo, mkoani Dar es Salaam, ambacho hivi sasa kinazalisha mabomba ya maji.**

**Hali hiyo inakinzana na dhamira ya mwasisi wake, Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere ambaye serikali yake ilikianzisha kwa lengo la kuzalisha zana za kilimo ili kuhakikisha wakulima wanakuwa na uhakika wa kuzipata kwa urahisi nchini na kwa bei nafuu. Endelea na sehemu ya mwisho ya ripoti hii...**

Kwa miaka 26 wafanyakazi wa kiwanda hicho wanasotea haki zao. Wanadai wameshaandika zaidi ya barua 40 kwa mamlaka mbalimbali nchini tangu mwaka 1998 bila mafanikio yoyote.

Hadi kiwanda kinabinafsishwa mwaka 1998, kilikuwa na wafanyakazi 508 wanaodai stahiki zao za malipo ya mishahara, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na posho nyinginezo.

Taasisi ambazo wamekuwa wakielekeza barua zao kushughulikia madai yao ni pamoja na Bunge na Ikulu. Hata hivyo wanadai hawajui tarehe ya kulipwa stahiki zao.

Katibu wa Kamati ya Ufuatiliaji Mafao ya Wafanyakazi wa Kiwanda cha UFI, Makamba Kigome, anasema wanachodai ni kupunjwa katika malipo ya mtumishi na familia zao - kwamba hayakulipwa kulingana na umbali wa kila mmoja anakotoka, pia kutozingatiwa ngazi ya mshahara wa mtumishi.

Madai mengine ni posho ya kufungasha mizigo; haikuwafikia watumishi licha ya kuwapo kwenye mchanganuo wa malipo ya UFI.

Kigome anataja hoja zingine ni kutofuatwa Mkataba wa Hali Bora Sehemu ya Kazi, malimbikizo kulipwa kwa kutofuata mabadiliko ya mishahara tangu Julai 1994 hadi Julai 1998, kutolipwa malimbikizo ya likizo badala yake walilipwa likizo moja pekee ya mwaka 1994.

Wafanyakazi hao pia wanadai posho ya kujikimu kwa kipindi cha miezi mitatu wakati wanasubiri kulipwa mafao ya kuachishwa kazi.

Mwandishi ameona nakala za barua 30 kati ya 41 ambazo wafanyakazi hao wanadai kuzielekeza kwa mamlaka mbalimbali za serikali kukumbushia madai yao.

Pamoja na taasisi zingine, barua hizo zimeelekewa kiwanda cha UFI wakati huo, Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma (PSRC) na uliokuwa uongozi wa UFI.

Mathalani, barua yenye kumbukumbu PSRC/1/13/143 ya Mei 2002 kutoka kwa Mtendaji Mkuu wa PSRC kwenda kwa Kamishna wa Kazi Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, ina maudhui ya madai ya waliokuwa wafanyakazi wa UFI, Linus Kupuya na wenzake 507.

Katika barua hiyo mnaelekezwa kuwa madai ya wafanyakazi hao yako nje ya utaratibu uliowekwa kwa mashirika yaliyobinafsishwa na serikali, hivyo hayatekelezeki.

"Sera iliyopo ni kwamba serikali inapolazimika kulipa mafao ya wafanyakazi badala ya kampuni ambayo ndio mwajiri wao, inalipa mafao ya kisheria tu.

"Ufafanuzi umekuwa ukitolewa mara nyingi kwa wahusika kupitia taasisi mbalimbali za serikali ikiwa ni pamoja na Waziri wa Fedha na Wizara ya Viwanda na Biashara," inasomeka barua hiyo ambayo mwandishi wa habari hii ameona nakala yake.

Katika barua hiyo, Mtendaji Mkuu wa PSRC anaeleza, "Malipo kwa mujibu wa stahili za kisheria ni mshahara wa mwezi mmoja ikiwa ni notisi ya kuachishwa kazi, malipo ya likizo isiyozidi ya kipindi cha mwaka mmoja, nauli ya likizo isiyozidi kipindi cha mwaka mmoja, nauli ya mfanyakazi na familia yake hadi sehemu alikozaliwa - ya mizigo na makazi.

"Pia gharama za kusafirisha mizigo kwa kiwango cha kanuni za uajiri, pamoja na malimbikizo ya mishahara ambayo mfanyakazi anakuwa ametumikia na hajalipwa."

Kwa mujibu wa Mtendaji Mkuu wa PSRC, serikali iliwasilisha michango ya akiba ya wafanyakazi ambayo ilikuwa haijawasilishwa kwenye mamlaka zinazohusika na waajiri wao.

Anaeleza katika barua hiyo kuwa wafanyakazi hao wanadai marupurupu yanayotokana na mkataba wa hiari kati yao na uongozi wa UFI, kiinua mgongo, gharama za ufungaji mizigo, notisi za kuachishwa kazi za miezi miwili na malimbikizo ya likizo zinazozidi moja.

"Kama utakavyoona madai ya aina hii hayapo kwenye orodha ya yale yanayostahili kulipwa na serikali chini ya sheria inayoongoza urekebishaji mashirika ya umma kwa sababu marupurupu ya mkataba wa hiari yanatakiwa yatokane na juhudi za uzalishaji za wafanyakazi wenyewe.

"Makubaliano haya ni kugawana sehemu fulani ya ziada inayotokana na uzalishaji mzuri. Wafanyakazi hawa walishalipwa mafao yao ya pensheni na mfuko wa pensheni wa mashirika ya umma kama inavyotakiwa.

"Mfanyakazi hawezi kuhusishwa na mpango zaidi ya mmoja wa pensheni au wa akiba ya uzeeni, na madai ya gharama za ufungaji mizigo na malimbikizo ya likizo zinazozidi moja hayapo katika utaratibu uliotajwa hapo juu," anaeleza Dk. H. Kavishe, Mtendaji Mkuu wa PSRC wakati huo, katika barua hiyo wakati akimjibu Kamishna wa Kazi wa wizara.

Katika barua yao ya Februari 14 mwaka huu waliyomwandikia Spika wa Bunge, Dk. Tulia Askon, waliokuwa wafanyakazi 271 wa kiwanda cha UFI, wanaeleza kuwa baada ya mchakato wa ubinafsishaji, walilipwa sehemu ya malimbikizo ya mishahara ya miezi sita kwa wafanyakazi 271 waliokuwa kazini na miezi 49 kwa wafanyakazi 237 waliokuwa likizo.

Katika barua ya Wizara ya Viwanda yenye kumbukumbu namba MIT-C/I.40/77 ya Agosti 16, 1998, Kaimu Waziri wa Viwanda na Biashara wakati huo, Kingunge Ngombale Mwiru (marehemu), alimwandikia barua Waziri wa Fedha wakati huo, Daniel Yona, akimweleza ulipaji wafanyakazi wa UFI utakavyofanyika.

Katika barua hiyo, Waziri Kingunge anasema, "Ninapenda nipendekeze kwako kwamba ulipaji mafao ya wafanyakazi ufanyike kwa awamu mbili; kwanza walipwe malimbikizo ya mishahara ili waweze kujikimu na baadaye walipwe mafao yao baada ya uchambuzi wa kina kufanywa na wataalamu."

Katika barua yao Februari 14 mwaka huu kwa Spika, waliokuwa wafanyakazi wa kiwanda hicho wanamweleza Spika kuwa:

"Malipo ya mafao hayakufanyika kabisa kwa wafanyakazi wote. Kwa wale wafanyakazi waliokuwa wametimiza masharti ya kuwa 'pensionable' (kulipwa mafao), yaani walikuwa wametumikia kiwanda zaidi ya miezi 120 (kwa vigezo vya Mfuko wa Pensheni kwa Mashirika ya Umma (PPF) na NPF) wakaingizwa katika mpango wa kulipwa pensheni kila mwezi 'kiainaaina', ambapo pia ukasitishwa na serikali kwa waliokuwa chini ya umri wa miaka 55."

Wafanyakazi hao wanasema katika barua hiyo kuwa wanachodai ni haki zao za msingi walizodhulumiwa.

Wanasema mafao wanayodai ni haki zao kwa kuwa walijiunga katika mifuko ya jamii ya PPF na NPF na wakachangia michango yao kutoka katika mishahara yao kwa mujibu wa sheria.

"Hatuombi kutoka nje ya hilo. Tunachohitaji ni mapunjo ya haki zetu pamoja na mafao yetu. Malipo hayo yalipwe kwa thamani ya Shilingi ya sasa," wafanyakazi hao wanadai.

Wanadai wamefikisha malalamiko yao sehemu zote husika, zikiwamo Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Fedha, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na Ofisi ya Waziri Mkuu. Hata hivyo, madai yao hayajafanyiwa kazi.

"Inatusikitisha na kutuumiza sana tunapoendelea kuzungushwa kupata stahiki zetu, hii imetufanya tuwe tegemezi na ombaomba katika jamii ambayo tuliitumikia kwa moyo na uadilifu mkubwa sana.

"Baadhi ya wenzetu wameshatangulia mbele ya haki kwa kukosa uwezo wa kujihudumia kimaisha na kimaendeleo wao na familia zao.

"Hivi tumekosa nini hata tuadhibiwe na kunyanyaswa namna hii kwa miaka zaidi ya 26 sasa? UFI na Urafiki ni viwanda vya Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alipata msaada toka China, tunaomba tulipwe kama walivyolipwa wenzetu wa Urafiki.

"Tunaomba utusaidie mahesabu haya baada ya kujiridhisha Bunge letu tukufu limshauri Rais Samia Suluhu Hassan atulipe madai yetu ambayo ni ya muda mrefu tuweze kupata malipo yetu kwani imekuwa muda mrefu sasa tumekuwa tukipeleka malalamiko yetu sehemu mbalimbali serikalini bila kupatiwa haki zetu za msingi.

"Tunaendelea kuishi katika hali ngumu inayohatarisha maisha yetu na familia zetu kutokana na uamuzi wa watu wachache kwa utashi wao binafsi," wafanyakazi hao wanalalama.

Katika barua hiyo, wafanyakazi hao pia wanadai UFI haikuonesha mali ambazo ni majengo, madeni waliyokuwa wanadai kwa kuwa kiwanda hakikuruhusiwa kuuza moja kwa moja kwa wateja bali waliuza kwa mkopo, pia fedha zilizobaki kwenye akaunti za kiwanda na bidhaa ambazo zilikuwa hazijaisha.



Makaravati yakiwa yameandaliwa kwa ajili ya ujenzi unaoendelea wa miundombinu ya mabasi yaendayo haraka katika Barabara ya Uhuru, eneo la Buguruni, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Serikali yapongeza benki kuanzisha kampuni ya bima

**Na Mwandishi Wetu**

KAMISHNA wa Uendelezaji Sekta ya Fedha nchini, Dk. Charles Mwamaja amepongeza Benki ya CRDB kwa kuanzisha kampuni tanzu ya bima ya CRDB Insurance Company (CIC).

Amesema kampuni hiyo itasaidia kwa kiasi kikubwa kuchangia ufikiwaji malengo ya serikali ya kuongeza ujumuishi wa bima kufikia asilimia 50 kwa Watanzania wenye umri wa kuanzia miaka 18 ifikapo 2030, mwaka ambao ni ukomo wa upimaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu.

Dk. Mwamaja aliyasema hayo jana alipozindua kampuni hiyo jijini hapa, ukiwa umepita mwaka mmoja tangu ipate leseni ya kutoa huduma za bima zisizo za maisha kwa Watanzania ili kuwalinda dhidi ya majanga yanayoweza kujitokeza.

Aliitaka CIC kutumia uzoefu na wigo mpana wa Benki ya CRDB kuwafikia wananchi hasa kwa kuzingatia kuwa benki hiyo imeenea katika halmashauri zote nchini.

Dk. Mwamaja ambaye alimwakilisha Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema sekta ya bima nchini bado ni changa lakini ina fursa kubwa za kuhudumia Watanzania iwapo elimu itatolewa na kampuni za bima kuwekeza katika ubunifu wa bidhaa zitakazogusa makundi mbalimbali ya wateja. Taifa litafikia lengo lake la kuongeza ujumuishi wa bima ifikapo mwaka 2030.

"Niwapongeze kwa ubunifu ambao mmeanza nao kwa kuja na bima ya kilimo kwa kushirikiana na ACRE Africa. Kilimo ni sekta muhimu katika uchumi wetu inayoajiri watu wengi zaidi. Iwapo mtafika mpaka vijijini mtatoa unafuu kwa wakulima wengi kulinda mazao na mifugo yao, jambo ambalo litasaidia kuwapa utulivu wa nafsi wakulima kupitia bima hii. Tunapaswa kujua kuwa huduma bora za bima ni msingi wa ustawi wa uchumi na kichocheo cha uwekezaji," alisema Dk. Mwamaja.

Kamishna wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), Dk. Baghayo Saqware alipongeza benki hiyo kwa kuwa taasisi ya kwanza fedha nchini kuanzisha kampuni tanzu ya bima.

Dk. Saqware alisema CIC inakwenda kutanua sekta ya bima nchini, jambo litakaloongeza ushiriki wa Watanzania katika kutumia huduma za bima.

Akieleza ujumuishi wa huduma za bima nchini, Dk. Saqware alisema hadi mwishoni mwa mwaka 2023, kulikuwa na watumiaji bima milioni 12 kutoka watu milioni sita waliokuwa wanatumia bidhaa hizo mwaka 2022.

Dk. Saqware alisema kuwa kupitia jitihada zinazotekelezwa na serikali, ikiwamo kuanzishwa kanuni ya bima za lazima, kunatarajiwa kuongeza ujumuishi maradufu kila mwaka kufikia lengo lililowekwa.

"Serikali pia imeanzisha konsotia ya bima ya mafuta na gesi, pamoja ya ile ya kilimo na mifugo. Ni imani yangu kuwapo kampuni kama CIC kutasaidia kufanikisha malengo kwa kuwekeza mitaji ili sehemu kubwa ya ada za bima ziwe zinabaki nchini," alisema Kamishna Saqware.

Aliitaka kampuni hiyo kuwekeza katika weledi kwa wafanyakazi na kusimamia sera na misingi iliyowekwa kisheria ili kuepukana na udanganyifu.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, Omary Mwaimu alimwambia Dk. Mwamaja kuwa lengo walilonalo ni kuifanya CIC kuwa kampuni ya bima chaguo nambari moja kwa Watanzania wote kupitia huduma bunifu na nafuu ambazo zitatoa fursa kwa makundi mbalimbali ya wananchi kujiunga na hivyo kuchochea ujumuishi wa bima nchini.

Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Abdulmajid Nsekela alisema kuanzishwa CIC ni mwendelezo wa utekelezaji wa azma yao kutanua wigo wake wa kufikisha huduma za fedha ikiwamo bima kwa Watanzania.

Nsekela alibainisha kuwa uamuzi huo umetokana na hali ya ufikiaji mdogo wa huduma za bima nchini huku akieleza kuwa mkazo mkubwa wa kampuni hiyo ya CIC umeelekezwa vijijini ambako wengi wako nje ya mfumo rasmi wa bima.

Mkurugenzi Mtendaji wa CIC, Wilson Mnzava alikaribisha mawakala na madalali wa bima, wateja pamoja na wadau wengine kuzitumia huduma za kampuni hiyo, akiahidi kuwa watapata utulivu wa maisha, nafsi, biashara na uchumi wao kipindi majanga yanapojitokeza.

CIC inakuwa kampuni tanzu ya nne ya Benki ya CRDB baada ya zile za CRDB Bank Burundi, CRDB Bank DR Congo na CRDB Bank Foundation.

Kampuni hiyo ya bima inatoa huduma za bima zisizo za maisha ikiwamo bima ya magari, bima ya nyumba, bima ya vyombo vya moto, bima ya biashara, bima ya usafirishaji, bima ya safari, bima ya ukandarasi na bima ya mitambo.

## Watumishi Afya wafa ajalini wakienda kusherehekea Idd

**Na Daniel Limbe,** CHATO

KUTOZINGATIA sheria kumetajwa kusababisha vifo vya watumishi wawili wa Idara ya Afya wilayani Chato, Geita waliofikwa na umauti kutokana na ajali ya barabarani juzi.

Watumishi hao walifariki duni baada ya gari aina ya Toyota Probox kugongana na mwendesha pikipiki aliyekuwa amebeba mtumishi mwenzake.

Kamanda wa polisi mkoani Geita, Safia Jongo, aliambia Nipashe kuwa ajali hiyo ilitokea juzi saa 12:15 jioni katika kijiji cha Mlimani Rubambangwe, wilayani Geita kwenye makutano ya barabara kuu ya Muganza-Buzirayombo na ile ya Chato-Biharamulo.

"Watumishi hao walikuwa na pikipiki wakitokea kwenye njia ndogo kuingia kwenye barabara kubwa pasipo kuchukua tahadhari, wakati mwenye gari alikuwa kwenye barabara kuu akielekea Chato," alisema Jongo.

Kamanda Jongo alitoa wito kwa madereva wote kuzingatia sheria za usalama barabarani ili kuepuka kutokea vifo visivyo vya lazima. Kila mmoja anapaswa kuelewa thamani ya maisha yake na watumiaji wengine wa barabara badala ya kusubiri kusimamiwa na askari wa Jeshi la Polisi.

Mganga Mkuu wa Hospitali ya Wilaya ya Chato, Dk. Madili Sakumi, akithibitisha kupokea miili ya watumishi hao wawili ambao ni Diana John muuguzi wa hospitali hiyo pamoja na Egidia Grevas (mtaalamu wa maabara wa Kituo cha Afya Bwina.

Baadhi ya marafiki wa marehemu hao walisema kuwa wawili hao walikumbwa na umauti huo wakati wakielekea nyumbani kwa Egidia kwa ajili ya kupata chakula kusherehekea sikukuu ya Eid Al-adha, wakitumia usafiri wao wa pikipiki.

## Wahariri wakunwa mradi wa EACOP

**Na Mary Geofrey**

WAHARIRI wa habari kutoka vyombo mbalimbali nchini wameonesha kuridhishwa na kuvutiwa na faida ambazo jamii na wananchi wa mikoa minane iliyopitiwa na Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) kutoka Uganda hadi mkoani Tanga.

Mradi huo unaotekelezwa katika eneo lenye urefu wa Km 1,443 kutoka Hoima, Uganda hadi Tanga, Tanzania, unapita katika mikoa minane ya Tanzania; Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga. Km 296 zimo ndani ya Uganda na 1,147 ni za Tanzania.

Wakizungumza mwishoni mwa wiki katika semina iliyoandaliwa na EACOP kwa ajili ya kuwaeleza maendeleo ya mradi ulipofikia na kuwaeleza faida za mradi huo, wahariri walipongeza kazi iliyofanyika, hasa kuzingatia maslahi ya Watanzania waliopitiwa na mradi.

Mhariri wa Brains Media na Mjumbe wa Kamati ya Utendaji wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Nevile Meena, alisema semina imefungua macho na kuwajengea uelewa wa pamoja wa mradi na kuweza kutoa taarifa sahihi kwa umma kuhusu hatua zote za maendeleo ya mradi.

"Kazi kubwa sana imeshafanyika katika maandalizi na wananchi wameshirikishwa ipasavyo katika eneo zima la mradi. Nikiri nimeweza kujionea mwenyewe na kiukweli nichukue nafasi hii kupongeza EACOP kwa kazi nzuri sana," alisema Meena.

Mhahari wa Gazeti HabariLeo linalomilikiwa na serikali, Mgaya Kingoba, alisema, "Kwa hatua ya awali tumeona fidia zimeshatolewa na tumeona tayari nyumba zaidi ya 400 zimeshajengwa.

"Mimi kama shuhuda ninaweza kusema mimi binamu yangu amelipwa fidia ya shamba lake pamoja mali zote zilizoko wilayani Handeni, mkoani Tanga."

Mhariri wa Kituo cha Runinga cha Channel Ten, Khamis Mkotya, pamoja na kupongeza mafunzo ya EACOP, alisema ni mnufaika wa moja kwa moja wa mradi huo kwa kuwa umepita katika Wilaya yake ya Chemba, mkoani Dodoma na kunufaisha wananchi wengi wakiwamo ndugu zake.

Akifunga semina hiyo kwa wahariri, Mkuu wa Mawasiliano wa EACOP upande wa Tanzania, Catherine Mbatia, alishukuru wahariri kwa kujitokeza kwa wingi kwenye semina, akiitaja itasaidia kuwa uelewa wa pamoja sambamba na kufahamu hatua mbalimbali za maendeleo ya mradi.

"Sisi kama EACOP tutafanya kazi kwa karibu sana na wahariri na waandishi wote wa habari kama wadau muhimu wa mradi huu kwani mkiuelewa ninyi, jamii na umma mzima wa Watanzania utauelewa," alisema Mbatia.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mauaji mtoto mwenye ualbino hayavumiliki

**BAADA** ya mtoto mwenye ualbino kutekwa mikononi mwa mama yake na kutoonekana kwa wiki kadhaa, taarifa zimeripoti kuwa amekutwa akiwa ameshafariki na kutupwa kwenye mtaro huku baadhi ya viungo vyake vikiwa vimekatwa.

Taarifa hizo zimepokewa na wengi kwa huzuni hasa ikizingatiwa kuwa aliyedhulumiwa maisha yake ni mtoto asiye na hatia.

Uchungu anaopitia mama wa mtoto huyo hauwezi kulinganishwa na kitu chochote ni jambo ambalo hataweza kulisahau katika maisha yake yote.

Vitendo vya kutekwa na hata kuuawa kwa watu wenye ualbino vikuwa vikijitokeza nchini na kuweka jamii hiyo katika hali ya wasiwasi.

Watu wenye ualbino wana haki ya kuishi kama wengine kama Katiba ya Jamhuri ya Muungano inavyosema.

Watu hawa wanawindwa hata wanapokuwa wamelala jambo linalowanyima haki ya kuishi kama binadamu wengine.

Matukio haya yanahusishwa na imani za kishirikina na baadhi ya waganga wa jadi wanatuhumiwa kuhusika kushawishi watu kufanya matukio hayo.

Kuhusishwa kwa baadhi ya waganga wa jadi kumedaiwa kutokana na kuwadanganya wateja wao kuwa viungo vya watu wenye ualbino vikitengenezewa dawa, wanapata utajiri wa haraka haraka.

Vitendo hivi vya mauaji ya watu wenye ualbino, kukatwa viungo na kutekwa vimedaiwa vikijitokeza wakati biashara za madini zikishamiri na kila wakati inapokaribia kipindi cha uchaguzi.

Ndiyo maana kumekuwa na imani kuwa vitendo hivyo vinafanyika kwa kuamini mambo ya nguvu za giza ambazo zinawaondolea watu wasiokuwa na hatia haki ya kuishi.

Kutekwa kwa mtoto mwenye umri wa miaka miwili mwenye ualbino (sasa ni marehemu), kulizua taharuki kubwa.

Mtoto huyo aliibwa kijijini kwao Buamula, mkoani Kagera akiwa mikononi mwa mama yake na watu wasiojulikana.

Kwanini matukio kama haya yaendelee kutokea nchini kila mara, huku baadhi ya wahalifu wakikamatwa na wengine kupata adhabu kali?

Matukio haya yanasababisha watu wenye ualbino kuomba ulinzi ili wakiwa kwenye shughuli zao au wakiwa kwenye makazi yao wasiwe na wasiwasi wa kuvamiwa na kufanyiwa vitendo vibaya.

Tanzania inasifika kwa kuwa nchi yenye amani na utulivu na wananchi wake wako huru kutembea bila kuwa na wasiwasi, lakini watu wachache wenye uroho wa utajiri wanataka kuitia doa kwa vitendo vya kinyama wanavyowafanyia binadamu wenzao.

Pamoja na wanaharakati wanaopigania haki za binadamu kupiga kelele kuhusu matukio hayo na kutaka watu wenye ualbino wasichukuliwe kama viumbe tofauti, bado watu wenye imani potofu wanaendeleza vitendo hivyo.

Serikali kwa kushirikiana na vyama vya watu wenye ualbino vinatoa elimu ya kupambana na matukio hayo na kuna wakati hali hiyo ilitulia, lakini yameanza kujitokeza tena kutokana na baadhi ya watu kutaka utajiri wa haraka bila kufikiria uhai wa watu wengine.

Unapomuua binadamu mwenzako kwasababu ya kutaka mali, huo utajiri utakuwa na raha nao? Hivi wanaofanya vitendo hivyo wana hofu ya Mungu kweli? Watu wote wanapaswa kupaza sauti kukemea unyama huo.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kimekuwa mstari wa mbele kutetea haki za binadamu na katika tukio hili la kutekwa kwa mtoto wa miaka miwili kimetaka serikali kupitia vyombo vyake vya ulinzi, mtoto huyo apatikane.

Pia, ni muhimu kila mtu kuweka ulinzi dhidi ya mwenzake ili yanapojitokeza matukio kama hayo iwe rahisi hatua kuchukuliwa haraka.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Siku Mtoto wa Afrika, walindeni sana watoto

Na Mwandishi Wetu

**WIKI** hii ni muhimu kwa malezi na usalama wa mtoto hasa ikizingatiwa Siku ya Mtoto wa Afrika inayoadhimishwa Juni 16 kila mwaka.

Shule za msingi na sekondari zimefungwa na masuala ya kusoma, kufurahia masomo katika mazingira mazuri pamoja na kufaulu, yamewekwa pembeni ili wanafunzi wafurahie likizo na mapumziko.

Wakati wa likizo pamoja na kufuatilia siku ya mtoto wa Afrika , usalama na ulinzi wao ni jambo linalohitaji wazazi,walezi na jamii kulipa umuhimu wa kipekee.

Ulinzi na usalama unagusa kila mmoja kuwaangalia kuanzia shuleni wanaposoma , mitaani wanapokaa na mambo muhimu wanayohitaji ili kuwasaidia wasome salama na wakue bila kukatiliwa.

Lakini juhudi hizi ziende pamoja na kuhakikisha kuwapo kwa huduma za kijamii kama maji, chakula na kulindwa iwe shuleni kwa darasa la nne na la saba, kidato cha pili na cha nne.

Ni lazima kufanya hivyo kwa sababu watoto wengi wanaathirika na ukatili wa kijinsia hasa mabinti ambao hupewa mimba utotoni, kutumiwa kingono na walimu au walezi na hata kuozwa yote hayo yanaweza kuchangiwa na ukosefu wa huduma za jamii, ulinzi na usalama.

Ukiangalia sekondari, huduma muhimu zinazozungumziwa hapa ili mtoto afanikiwe ni kama chakula, mabweni, maji, hospitali na usafiri.

Ili kumlinda mtoto wa Afrika na Watanzania ni lazima kwa kiasi tujue kuwa ukosefu wa bweni huwalazimisha wasichana kupanga nyumba mitaani, wakati kuishi bila maji kunachangia kujihimu alfajiri kwenda kisimani au mtoni au usiku wa manane kusaka maji yote yakiwatumbukiza kwenye mikono ya wanyanyasaji.

Kusoma pasipo na chakula kunamaanisha njaa isiyovumilika, matokeo yake ni binti kufanya lolote bila kujali itakuwaje ili apate chakula, asife njaa.

Yote hayo na mengine mengi huchangia mimba, utoro na watoto kuchukia shule, bila kurekebisha hali hiyo mtoto wa Tanzania atakuwa duni licha ya juhudi kumtunza mtoto wa Afrika.

Ni vyema wazazi, walezi na wadau wa elimu watatue matatizo hayo yanayohusiana na huduma za msingi ili kupunguza tatizo linalohusiana na kukwamishwa kusoma kutokana na matatizo hayo kila mwaka.

Usalama na ulinzi wa watoto unakwenda mbali zaidi kwa kuwasimamia na kuwaepusha na athari za utandawazi ni kwa sababu umewaharibu wa sekondari na msingi kwa vile wamekuwa wateja wa mitandaoni kujifunza'maovu.'

Wanatumia simu kuangalia picha kwenye YouTube zenye maudhui ya ngono, kujifunza masuala mengine makubwa kuliko mri wao, wapo wanaojifunza na kufanya uhalifu.

Utandawazi unawatumbukiza katika kupenda muziki wa disko usiku, lakini wale wanaokaa mbali na nyumbani au waliopanga mitaani ni wapenzi wa mikesha ya harusi na ngoma.

Wakati mwingine ni waraibu wa sinema zinazoonyeshwa kwenye vibanda umiza mitaani.

Watoto hawa wanapokosa uangalizi wanaweza kuishi kwenye nyumba za sinema mchana au vibanda umiza, mabinti wanaweza kuzamia kwenye mikesha au wakaranda mitaani kwa maelezo kuwa hakuna mabweni shuleni wanalazimika kupanga.

Wengi huishia kushawishiwa na kutumbukia kwenye vitendo vya kuwakwamisha kimasomo.

Watoto wanaingia mitegoni wanapokwenda kwenye mabanda yanakoonyeshwa video mchana na kukutana na watu wanaowalipia kiingilio, kuwapa chips na soda kitakachofuata ni ulaghai na hadaa za ngono, zinazoweza kuwaondoa shuleni, kupata mimba na kuzitoa utotoni na kuambukizwa magonjwa.

Pamoja udanganyifu huo mabinti wanaweza kuingizwa mtegoni na walimu ambao ama kwa kisingizio cha kuwafundisha twisheni au kuwaomba wasaidie kazi za nyumbani wanawabaka au kuwashawishi kuingia kwenye ngono.

Ni vyema kuwaangalia watoto wasiwe waathirika wa kutafuta fedha za kujikimu kwa kulazimishwa kufanyakazi za kuosha vyombo, kutafuta kuni , kufua nyumbani kwa walimu na wanavijiji au wanajamii ili kupata fedha za kuishi na kununua mahitaji ya msingi ya kitaalamu na maisha.

Wazazi, walezi , jamii na asasi za kiraia waanze kufuatilia na kuhoji sababu za wasichana au wanafunzi kuzurura, kufanya mambo yanayokwenda kinyume na taratibu.

Mambo yasiishie hapo taarifa zifikishwe polisi, dawati la jinsia, kwa watendaji wa elimu na hata viongozi wa siasa ili kupata ufumbuzi.

Jamii isikae kimya maana kudhalilisha watoto hakuwezi kukoma kama jamii itaendelea kukaa kimya.

# CTI wapongeza bajeti miradi kimkakati

**Na Joseph Mwendapole**

SHIRIKISHO la Wenye Viwanda nchini (CTI), limepongeza bajeti kuu ya serikali kwa kuweka mambo muhimu ambayo yatachochea ukuaji wa viwanda nchini.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi wa shirikisho hilo, Leodegar Tenga, wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema serikali imekuwa sikivu kwa wenye viwanda na kila wanapokuwa na jambo wanafunguliwa milango ya majadiliano na hakuna jambo la wenye viwanda ambalo linakwama.

Alisema wenye viwanda wamefurahia bajeti ya serikali kwa kuzingatia uendelezaji wa miradi ya kimkakati kama Reli ya Kisasa (SGR) ambayo alisema itasiadia kwa kiwango kikubwa kukuza viwanda vya ndani kuzalisha kwa wingi bidhaa.

Alisema miradi kama SGR inasaidia kukuza uchumi kwa kuwa viwanda vitazalisha kwa wingi na bidhaa kusafirishwa kwa urahisi tofauti na sasa usafirishaji umekuwa ukisababisha bei kupanda.

"Nchi ambayo iko makini inaendeleza miradi mikubwa kama ya ujenzi wa reli, barabara, miradi ya maji kama kuendeleza miradi ya kimkakati barabara maji, bandari kwasababu huwezi kuendeleza viwanda kama huna umeme au una matatizo ya usafirishaji," alisema.

"Mfano bei ya mfuko wa saruji hapa Dar inaweza kuwa shilingi 16,000 au 17,000, lakini bei ya kuubeba mpaka Mwanza ni kati ya Sh 10,000 hadi 12,000 kwa hiyo mtu ananunua mfuko wa saruji hapa kwa 16,000, lakini mpaka kuufikisha Mwanza unauzwa shilingi 28,000," alisema.

"SGR itapunguza gharama ya usafirishaji na bei ya bidhaa itapungua sana na itasaidia viwanda vya ndani kukua na kuongeza mapato na ni vizuri serikali inapofanya vizuri sekta binafsi tuseme kwamba inafanya vizuri," alisema.

Tenga alisema bajeti ya mwaka huu inakusudia kuhamasisha mapato ya ndani zaidi ikilinganishwa na bajeti ya 2023/24.

Alisema jambo muhimu katika bajeti ya mwaka huu ni serikali kufanya mageuzi mbalimbali ya muundo wa kodi, ada, tozo na marekebisho ya sheria na kanuni ili kuboresha mazingira ya biashara.

Alisema marekebisho ambayo yamependekezwa kuhusiana na sekta ya viwanda ni katika ongezeko la thamani VAT, ushuru wa bidhaa, ada na tozo za wakala pamoja na ushuru wa forodha.

Aidha, alisema baadhi ya hatua chanya ni pamoja na kuanzishwa kwa tozo ya maendeleo ya viwanda kwa bidhaa zinazotoka nje yenye lengo la kulinda viwanda vya ndani, kuchochea uwekezaji na kuongeza mauzo ya nje; kupunguza ada na tozo zinazotolewa na vyombo vya udhibiti ili kupunguza gharama za uzalishaji.

Alisema pia wamefurahishwa na kupunguzwa kwa ushuru wa forodha kwenye malighafi za viwandani na pembejeo za uzalishaji ili kuongeza ushindani wa viwanda vya ndani na kutozwa ushuru wa VAT kwenye bidhaa za nguo zinazotengenezwa kwa pamba inayolimwa hapa nchini ili kuchochea uwekezaji katika viwanda vya nguo vya ndani.

Alisema hatua za kodi zilizopendekezwa zinalenga kusaidia viwanda vya ndani katika kupunguza gharama za uzalishaji, kuhimiza matumizi ya vifaa vya ndani, kuongeza ushindani na kukuza ukuaji wa uchumi.




Mkurugenzi wa Shirikisho la Wenye Viwanda (CTI), Leodegar Tenga (katikati), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu maoni ya wenye viwanda kwenye bajeti kuu ya serikali. Kulia ni Mkurugenzi wa Sera, Akida Mnyenyelwa na Mtaalamu wa Sera za Viwanda, Isack Msungu. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Majaliwa: Serikali itahakikisha wananchi wanapata maendeleo

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imedhamiria kuhakikisha wananchi wote wanapata maendeleo na huduma mbalimbali za msingi kwa wakati na maeneo yao ya makazi.

Kauli hiyo imetolewa hivi karibuni na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa wakati akifungua Mkutano Mkuu wa 14 wa Taasisi ya Maboresho ya Serikali za Mitaa Tanzania (TOA) uliofanyika katika Ukumbi wa Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha (AICC), jijini Arusha.

Alisema watu wote wanatambua majukumu makubwa yanayotekelezwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya wananchi kujiletea maendeleo kwa kutumia rasilimali zinazowazunguka na kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi.

Alisema kwa kutambua kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa ndiyo zinazosimamia maendeleo ya wananchi katika ngazi ya msingi, serikali imekuwa ikitekeleza majukumu yake kupitia dhana ya ugatuaji wa madaraka kwa namna mbalimbali tangu nchi ilipopata Uhuru 1961.

Katika kuhakikisha dhamira ya serikali ya kuwaletea wananchi maendeleo inatimia, Waziri Mkuu amewataka watumishi wa umma nchini kote wawatumikie wananchi ipasavyo na wahakikishe wanaondoa urasimu kwa kutowasumbua wanaokwenda kupata huduma za kiserikali katika ofisi zao.

"Epukeni tabia ya kuomba na kupokea rushwa kwani inaharibu maendeleo. Tusitumie maneno magumu kwa wananchi wetu maana eneo hili bado ni changamoto, kwa mfano tunalishughulikia au bado tupo kwenye mchakato, tunafanya tathmini, upembuzi yakinifu, tumieni lugha rahisi."

Pia, Waziri Mkuu aliwataka watumishi hao wazingatie taaluma zao na watoe ushauri kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma, wafike sehemu ya kazi kwa muda uliopangwa na watumie muda huo kufanya kazi za serikali na waepuke kuwa na migongano ya maslahi katika kutekeleza majukumu na kusimamia rasilimali za umma.

"Viongozi wote tuwahudumie wananchi kwa heshima, staha, unyenyekevu na umakini mkubwa ikiwa ni pamoja na kuwapa majibu sahihi ya maswali yao na majawabu sahihi ya kero zinazowasumbua. Toeni ufafanuzi au maelekezo juu ya masuala yatokanayo na sheria, kanuni na taratibu za serikali kwa haraka, uwazi na bila upendeleo wowote au ubaguzi wa aina yoyote."

Pia Waziri Mkuu amewataka wakurugenzi wa halmashauri wahakikishe wanakuwa na mifumo madhubuti ya ukusanyaji na usimamizi wa mapato pamoja na kuweka mkakati wa udhibiti wa mali zilizopo ndani ya halmashauri na mapato watakayoyapata wayaelekeze katika kukamilisha miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika halmashauri zao.

Kadhalika, Waziri Mkuu aliwasisitiza watumishi wa umma kuzingatia nidhamu na maadili ya utumishi wa umma. "Tufanye kazi kwa bidii na kujitolea kwa ajili ya maendeleo ya taifa letu. Hivyo ni lazima tuhakikishe kuwa kila mtumishi anazingatia nidhamu na maadili katika utekelezaji wa majukumu yake."

Aliwasihi washiriki wote kuchangia kikamilifu katika majadiliano na kutoa mapendekezo yatakayoimarisha utendaji kazi na kuleta mabadiliko chanya katika serikali za mitaa. Tukiungana pamoja, tunaweza kufanya mabadiliko makubwa na kuleta maendeleo endelevu kwa taifa letu.

Mafunzo na uendelezaji wa stadi ni sehemu muhimu sana ya kuhakikisha kuwa nguvukazi yetu inakuwa na ujuzi na maarifa yanayohitajika katika kutoa huduma bora. Ni lazima viongozi tuwe na mikakati madhubuti ya kutoa mafunzo yanayolenga mahitaji halisi ya watumishi wetu ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na ubunifu.

Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI, Dk. Festo Dugange, alisema wizara hiyo itaendelea kufanya maboresho ya utendaji kwa watumishi wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ili kutimiza dhamira ya Mheshimiwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ya kuwaletea maendeleo Watanzania.

Kuhusu TOA, Dk. Dugange alisema taasisi hiyo imesaidia kuboresha utendaji wa watumishi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na Tawala za Mikoa kupitia mafunzo yanayotolewa ambayo yamekuwa na tija kwa taifa kwa kuwa yameimarisha ukusanyaji wa mapato kupitia ushuru, ada na tozo mbalimbali.

Awali, Mwenyekiti wa TOA Taifa, Albert Msovela, alisema lengo kuu la taasisi hiyo ni kuchangia ongezeko la ushiriki wa wananchi katika masuala yote yanayohusiana na fedha, utawala na utoaji wa huduma katika misingi ya ugatuzi wa madaraka (Decentralization by Devolution - D by D) na kutetea dhana ya ugatuaji wa madaraka katika ngazi zote za serikali.

Alisema lengo jingine ni kuwaleta pamoja wadau wote wa serikali na sekta binafsi ili kubadilishana uzoefu katika utekelezaji wa dhana ya ugatuzi wa madaraka katika maboresho ya serikali za mitaa nchini pamoja na kukuza uwekezaji katika ngazi za msingi (Local Economic Development - LED).

Akizungumzia mafanikio ya TOA, Msovela alisema tangu kuanzishwa kwa taasisi hiyo mafanikio mbalimbali yamepatikana ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa fedha za maendeleo kwa ajili ya kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi katika ngazi za msingi, kuwapo kwa mifumo ya kusimamia matumizi ya fedha za serikali.

Alitaja mafanikio mengine kuwa ni pamoja na upangaji mipango katika Halmashauri na kuanzishwa kwa mfumo wa Ruzuku ya Maendeleo kwa Serikali za Mitaa (Capital Development Grant - CDG) kama sehemu ya ugatuzi wa masuala ya kifedha. "Fedha kutoka mfuko huu zilisaidia sana katika kutekeleza miradi ya maendeleo ambayo wananchi wamechangia ngvu zao.

# NBAA, PSPTB zashauriwa kushirikiana na vyuo vikuu

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

BODI ya Uhasibu na Ukaguzi (NBAA) na Bodi ya Ununuzi na Ugavi (PSPTB), zimeshauriwa kushirikiana na vyuo vikuu nchini katika kutoa elimu ya awali kwa wanafunzi itakayowasaidia kuona umuhimu na faida za bodi hizo na kujiunga kwa kuongeza ufanisi wa taaluma zao.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya vijana inayohusika na kutoa elimu na mitihani ya bodi (Suyoo vijana Resolution Group), James Suka, alisema hayo jana wakati taasisi hiyo ilipokutanisha wataalamu kutoka fani za biashara, wahasibu, wakaguzi wa hesabu wa ndani na nje na ununuzi, uchumi na masoko kwenye warsha ya kuleta mahusiano kwa wadau hao na wanafunzi.

Suka alisema licha ya kuwa na wanafunzi zaidi ya 200 anaamini elimu ingeanza kutolewa kwenye vyuo vinavyodahili na kutoa wanafunzi kila mwaka nchini itasaidia wengi zaidi kujitokeza na kupata elimu wanapohitimu vyuoni.

Alisema wameamua kufanya warsha hiyo kila mwaka ili kusaidia kutoa uelewa kwa wanafunzi ya uwapo wa bodi hizo kutokana na changamoto ya uelewa mdogo wa wanafunzi kuhusu mitihani ya bodi na taratibu zake.

Hata hivyo, aliwataka wanafunzi kutambua kuwa wanapaswa kuitumia bodi katika kujiendeleza sababu bodi inachukua kada zote na hatua mbalimbali za elimu kuanzia kidato cha nne kupitia wavuti ya bodi.

"Sisi hutoa elimu kwa wafanyakazi kutoka ofisi za umma na binafsi Mkoa wa Morogoro na wanafunzi wanaosoma masomo ya biashara katika vyuo vikuu vilivyopo mkoani hapa, na ndio maana warsha hii leo imehudhuriwa na washiriki zaidi ya 300 kutoka maeneo hayo ikiwamo vyuo vya Jordan, St. Joseph, SUA na Mzumbe," alisema.

Ofisa Mwandamizi wa Huduma na Elimu kwa mlipakodi kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mkoa wa Morogoro, Emmaculate Chaggu, alisisitiza wafanyabiashara kutoa risiti kwa hiari na kuepuka kupata adhabu ikiwamo kutozwa faini kwa manufaa ya umma.

"Tumepata taarifa na malalamiko kadhaa kutoka wateja kuwa muuzaji akidaiwa risiti yeye naye anamdai mnunuzi amuongezee hela ili aweze kumpa risiti halali anayoitaka, tunasisitiza wanunuzi mkikumbwa na changamoto hiyo ileteni, tutawachukulia hatua ya kuwafikisha mahakamani na hata kuwalipisha faini kubwa," alisema Chaggu.

Naye mmoja wa washiriki, Ruth Samson, aliishukuru kwa elimu wanayoendelea kuwapatia huku wakiwakutanisha na wadau mbalimbali wa biashara na ana imani wanaweza kuwasaidia kufikia malengo waliyokusudia.

# Mke wa Rais ataka ushirikiano usalama wasichana Z'bar

**Na Mwandishi Wetu**

MKE wa Rais wa Zanzibar, Mama Mariam Mwinyi amesema suala la kumkomboa msichana wa Zanzibar linahitaji ushiriki wa taasisi za umma, binafsi na jamii kwa jumla wakiwamo wazazi na walezi, kwa ajili ya kuhakikisha wanakuwa salama.

Aidha, amesema wasichana wana haki ya kupata fursa sawa ya elimu kama wavulana kwa kuwa nao ni walezi wa familia na jamii kwa ujumla.

Mama Mariam Mwinyi ambaye pia ni Mwenyekiti wa Bodi ya Taasisi ya Zanzibar Maisha Bora Foundation (ZMBF), aliyasema hayo katika viwanja vya Shamata, Shehiya ya Majenzi, Wilaya ya Micheweni, Mkoa wa Kaskazini, Pemba, kwenye hafla ya ugawaji wa taulo za kike kwa wanafunzi wa kike wa Skuli ya Sekondari ya Micheweni kwaajili ya hedhi salama.

Pia Mama Mariam ameisifu Taasisi ya Lady Fatma ya Korea ya Kusini kwa kuunga mkono jitihada na malengo ya mradi wa Tumaini Initiative wa Zanzibar Maisha Bora Foundation ya kumkomboa mtoto wa kike wa Zanzibar kwa kutengeneza taulo za kike 1,500 na kila moja zikiwamo tano ndani.

Alisema taulo hizo zimewakomboa wasichana wengi kupata haki yao ya elimu kwa kuondoa hofu iliyowatafuna muda mrefu walipokuwa kwenye siku zao za kila mwezi.

Mama Mwinyi alisema ugawaji wa taulo hizo kwa wasichana wa Zanzibar ni endelevu wa kuwafikia wasichana wote nchi nzima ili kuondosa changamooto inayowakumba wengi wanaoshindwa kuhudhuria masomo yao wakiwa kwenye siku zao za mwezi.

Akizungumza kwenye hafla hiyo, Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Ali Abdul Gulam Hussein, aliipongeza Taasisi ya Zanzibar Maisha Bora Foundation kwa jitihada zake za kuendelea kumkomboa mtoto wa kike wa kizanzibari kwenye hifadhi ya hedhi salama.

Pia, alisema taasisi hiyo inaunga mkono juhudi za serikali kupitia kampeni yake ya kumrejesha mtoto wa kike skuli ambayo inashirikiana na Qatar na Shirika la kimataifa la UNICEF pia kusaidia kupunguza utoro kwa wanafunzi.

Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, Salama Mbarouk Khatibu, pia aliipongeza taasisi ya Zanzibar Maisha Bora Foundation kwa jitihada zake na kuendelea kutoa huduma bora za jamii, ikiwamo elimu na afya hasa kwa watu wa mkoa huo.

Alisema hivi karibuni taasisi hiyo imewafikia wana-Kaskazini Pemba 20303 baada ya kuweka kambi ya matibabu bure mkoani humo na kwamba wananchi 9,099 walipata matibabu.

Mratibu wa Taasisi ya Zanzibar Maisha Bora Foundation, Gulam Abdul Karim, alisema lengo la mradi wa Tumaini Initiative wa taasisi hiyo ni kutatua changamoto za hedhi kwa wanafunzi wote wa kike wa Zanzibar.

Taasisi hiyo ilianzishwa mwaka 2022 na mwaka jana ilizindua mpango mkakati wake wa miaka mitatu na mradi wa Tumaini kitambao hadi sasa umefanikiwa kuzalisha taulo za kike zaidi ya 5,000 zilizosambazwa kwa wasichana 1,500 wa shule za msingi na sekondari maeneo ya Unguja na Pemba.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

Tarehe: 19 Juni 2024

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati na Maji (EWURA) inawatangazia Wananchi wote kuwa itauza kwa njia ya mnada wa hadhara samani na vifaa mbalimbali chakavu katika ofisi yake ya Kanda ya Mashariki-Dar es salaam katika Jengo la PSSSF Millenium Tower-Makumbusho sehemu ya maegesho ya magari chini (Basement 1) jijini Dar es Salaam kwa tarehe kama ilivyoonyeshwa hapa chini.

Mali zitakazouzwa ni pamoja na Samani za Ofisi, vifaa vya Tehama na Vifaa vya Ofisi ambavyo vilikuwa havitumiki kutokana na uchakavu wake au kushindwa kutumika kutokana na mabadiliko ya technolojia.

**Mnada utafanyika siku ya Alhamisi:**

| TAREHE | KITUO/ENEO | AINA YA MALI ZITAKAZOUZWA |
|---|---|---|
| 25/06/2024 | EWURA Kanda ya Mashariki<br>Jengo la PSSSF Millenium Tower-Makumbusho,<br>Sehemu ya maegesho ya magari, ghorofa ya chini (Basement 1) Dar es Salaam, | (1) Samani za Ofisi:meza, viti, kabati, file cabinet, nk;<br>(2) Vifaa vya Tehama: Printer, Scanner, UPS, monitor, nk; na<br>(3) Vifaa vya Ofisi: Money counting machines, paper shredders, water boilers, microwaves, nk. |

**MASHARTI YA MNADA**
1. Vyombo / Vifaa vitauzwa kama vilivyo na Mahali vilipo.
2. Mali zote mnunuzi atalazimika kulipia asilimia mia moja (100%) siku ya mnada.
3. Malipo yote kwa Chombo/Kifaa kitakachonunuliwa yatafanyika kwa kutumia namba ya malipo (control number) itakayotolewa kwa mfumo wa GePG.
4. Ruhusa ya kuangalia Mali itatolewa muda wa kazi kuanzia saa 4.00 asubuhi hadi saa 9.00 Alasiri siku mbili (02) za kazi kabla ya tarehe ya mnada husika.
5. Mnada utaanza saa 4.00 asubuhi.
6. Namba za mawasiliano +255765546649/ +255753 641044 +255 22 2923515-6

**Dr. James A. Mwainyekule**
**MKURUGENZI MKUU**

Jengo la EWURA, 3 Mtaa wa EWURA , 41104 Tambukareli, S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania
Simu: +255 26 2329002 – 4 • Nukushi: +255 26 2329005 • Barua Pepe: info@ewura.go tz



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

## TAARIFA KWA UMMA

**(Imetolewa chini ya kifungu cha 19 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania na Kanuni ya 20 (4) ya Kanuni za Mafuta Biashara ya Jumla, Uhifadhi, Rejareja na Matumizi Binafsi), Gazeti la Serikali Toleo Na. 150 la 2022)**

**TAARIFA** inatolewa kwa umma kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea maombi ya kubadili umiliki wa leseni na jina la kituo cha mafuta kama ifuatavyo: -

**Jina la awali la kituo:** Som Petroleum (T) Limited-Pingo
**Nambari ya Leseni:** PRL-2022-005
**Mahali Kituo kilipo:** Kiwanja Na. 1, Eneo la Pingo, Wilaya ya Chalinze, Mkoa wa Pwani
**Jina linalopendekezwa:** Iftin Oil Co. Limited
**Mmiliki wa awali:** Som Petroleum (T) Limited
**Mmiliki mpya:** Iftin Oil Co. Limited

Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi dhidi ya mabadiliko ya umiliki na majina ya leseni tajwa hapo juu, afanye hivyo kwa maandishi na kuwasilisha EWURA kwa anwani iliyotajwa hapa chini ndani ya siku kumi na nne tokea tarehe ya tangazo hili.

**Imetolewa na**
**Mkurugenzi Mkuu,**
**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji – EWURA**

Jengo la EWURA, 3 Mtaa wa EWURA , 41104 Tambukareli, S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania
Simu: +255 26 2329002 – 4 • Nukushi: +255 26 2329005 • Barua Pepe: info@ewura.go tz

## ‘Wapeni watoto urithi wa elimu’

**Na Allan ISACK,** MANYARA

MKUU wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga, amewataka wazazi na walezi kuwapa urithi wa elimu watoto wao kwa manufaa yao ya badaye.

Sendiga alitoa kauli hiyo juzi kwenye Kituo cha watoto wenye mahitaji maalumu cha Light In Afrika kilichopo mji wa Mirerani wilayani Simanjiro, ikiwa ni sehemu ya Maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika.

Alisema urithi wa elimu ni bora zaidi kuliko wa mali kwani kwa sababu mtoto hawezi kufilisika tofauti na mali au rasilimali inayouzika.

Sendiga, alisema jamii inapaswa kuishi kupitia kauli mbiu ya siku ya watoto inayosema elimu jumuishi kwa watoto, izingatiwe maarifa, maadili na stadi za kazi.

“Unapompa mtoto urithi wa elimu unakuwa umewekeza jambo kubwa kwenye maisha yake na hata akiwa mkubwa ataitumia elimu hiyo kwa manufaa yake na jamii inayomzunguka,” alisema.

Mkuu huyo wa mkoa, alikikabidhi kituo hicho kwa ajili ya kununulia mahitaji muhimu.

“Tumetoa sadaka yetu kwa watoto hawa ili waweze kununuliwa mahitaji muhimu na tunawapongeza wasimamizi na walezi kwa namna mnavyokuwa nao,” alisema.

Mwenyekiti wa Chama cha Wachimbaji Madini Mkoa wa Manyara (MAREMA), Justine Nyari amempongeza mkuu huyo wa mkoa huo kwa kushiriki siku hiyo kwenye kituo hicho.

“Mkuu wetu wa mkoa wa Manyara amefanya jambo sahihi kujumuika nao kwani hawa watoto wa kituo hiki ukiwaona utatoa machozi hivyo wanapaswa kusaidiwa,” alisema Nyari.

Mkazi wa Mirerani, Shujaa Baruti, alisema amekuwa akijumuika na watu wanaotaka kutoa sadaka kwa watoto hao.

“Unapaswa kumshukuru Mungu kwa zawadi ya uzima kwa watoto ukiwaona watoto wa kituo hicho utatoa machozi kwa namna walivyo ila nawapongeza wanaowalea na kuwapa uangalizi wana moyo mkunjufu,” alisema Baruti.

**“Unapompa mtoto urithi wa elimu unakuwa umewekeza jambo kubwa kwenye maisha yake na hata akiwa mkubwa ataitumia elimu hiyo kwa manufaa yake na jamii inayomzunguka,” alisema.**



Mkazi wa Mtaa wa Mdote Wilaya ya Muheza, Tanga, Abdallah Ramadhani, akiwa amebeba ndoo katika baiskeli yake juzi, akienda kuchota maji katika bwawa la Muheza Estate kutokana na ukosefu wa maji safi na salama kwa afya za binadamu wilayani hapo. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Madiwani wawaangukia wadau mfumo ukusanyaji mapato

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Karatu mkoani hapa, wamewaomba wadau kushirikiana ili kufanikisha kufungwa kwa mifumo ya kielektroniki ya ukusanyaji mapato (GoTHOMIS) katika vituo vya afya 41 vya wilaya hiyo.

Wito huo ulitolewa jana na madiwani hao katika baraza maalum la kujibu hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Diwani wa Kata ya Baray, Elitumaini Magnus, alisisitiza kuwa ufungwaji wa mifumo hiyo utaongeza kasi ya ukusanyaji mapato.

“Kwa sasa halmashauri hii imefunga mfumo huo katika vituo vya afya saba tu, vituo 34 bado havijafungwa,” alisema.

Mganga Mfawidhi wa Wilaya ya Karatu, Dk.Victor Kamazima alithibitisha vituo saba kufungwa mfumo huo na 34 havijafungwa.

“Mwaka huu wa fedha (2023/44) kabla haujaisha tumetenga shilingi milioni 34 kwa ajili ya kununua vifaa vya awali ikiwamo kompyuta ili tuanzie hapo,” alisema.

Dk. Kamazima alisema kwa mwaka ujao wa fedha wa 2024/25, wametenga Sh. milioni 43 kwa ajili ya kufunga vifaa vya kisasa kwa vituo vilivyobaki.

Alisisitiza kuwa mchakato wa kufunga mfumo huo unaendelea kadri bajeti itakavyoruhusu kulingana na mapato wanaokusanya katika kila kituo cha afya.

Katibu Tawala Mkoa wa Arusha, Missaile Musa, aliagiza idara ya elimu msingi na sekondari kutoa uwiano sahihi wa idadi vitabu vya kiada na ziada ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi kujisomea.

Musa aliagiza hadi Septemba mwaka huu mfumo huo ufungwe ili kudhibiti upotevu wa mapato ya serikali.

Vilevile aliagiza madeni ya watumishi na wazabuni yalipwe ili kuondoa malalamiko kwa watoa huduma katika wilaya hiyo.

“Zingatieni utunzaji wa kumbukumbu za wadaiwa wenu maana kuna mahali ukifuatilia kumbukumbu za madeni wanayodai wazabuni mengine huyaoni, hivyo hakikisheni mnalipa mnayodaiwa,” alisema.

Mweka Hazina wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Liberatus Kazungu, alisema halmashauri hiyo imepata hati safi kwa kipindi cha miaka minne mfululizo, huku hoja zikiwa ni 22, hoja 17 zikiwa ni za mwaka 2022/23 na hoja 12 ndio zilizobaki na 11 zimetekelezwa na moja ipo katika hatua ya utekelezaji.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Dadi Kolimba, alitaka usimamizi mzuri wa kazi na kufuata hoja zilizopo awali, ikiwamo hoja za magari kutengenezwa na mifumo ya afya kufanya kazi na ushauri wa Mkaguzi wa ndani wa hesabu uzingatiwe.

“Lazima kuhakikisha mnaimarisha kitengo maalumu cha ukaguzi ili kupunguza hoja na maoni ya mkaguzi wa ndani,” alisema.

# Wapatiwa kitoweo sherehe ya Eid

**Na Cynthia Mwilolezi,** MANYARA

WATOTO yatima, wajane, wahitaji na taasisi zilizopo mji mdogo wa Mirerani Wilaya ya Simanjiro mkoani hapa wamepatiwa nyama kwa ajili ya kusherehekea Sikukuu ya Eid El Adha.

Msaada huo ulitolewa juzi na kusimamiwa na taasisi ya kijamii ya Akhsante Foundation Tanzania baada ya kuchinja ng’ombe 350, kondoo na mbuzi 1,800.

Mkurugenzi wa taasisi hiyo, Katada Hashimu Kimaro alisema kuwa:

“Tunatarajia kukamilisha shughuli hii kwa muda wa siku mbili kwa kuhakikisha walengwa wote wanapata nyama kwa ajili ya kusherehekea Idd,” alisema Kimaro.

Alisema wajane, yatima, vituo vya watoto wenye uhitaji na taasisi za eneo hilo wamenufaika na msaada huo.

Mmoja wa wakazi wa Mirerani, Asia Juma, alisema ameshereheka sikukuu hiyo kwa kula nyama ya mbuzi na wanawe baada ya kupatiwa na shirika hilo.

“Sisi wajane tumeshukuru kwa kupatiwa msaada huu ambao kwa namna moja au nyingine utatusaidia katika kusherehekea sikukuu hii,” alisema.

Ofisa Mtendaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mirerani, Isack Mgaya, alisema shughuli hiyo imefanyika kwa utaratibu waliopanga waandaaji kwa baraka zao.

“Walitushirikisha nasi tukawapa ushirikiano kwa kuhakikisha idara zote zinazohitajika zinashiriki ili jamii iweze kutimiza haja zao,” alisema.





# Makandarasi waagizwa kuandika mabango ya ujenzi kwa Kiswahili

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MAKANDARASI mkoani Shinyanga wameagizwa kutumia lugha ya Kiswahili kwenye mabango ya miradi ya ujenzi wanayotekeleza kwa manufaa ya wananchi.

Agizo hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki iliyopita wilayani hapa na Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha wakati akikagua ujenzi wa mradi wa barabara yenye urefu wa kilomita 12 ya uboreshaji wa miundombinu ya miji nchini (TACTIC).

Macha alifafanua kuwa ametoa agizo hilo kutokana na makandarasi kutumia Kingereza kwenye mabango yakionyesha ujenzi wa mradi unaendelea, isipokuwa neno moja tu UKIMWI linaandikwa Kiswahili.

Alisema mabango yanapoandikwa lugha ya kigeni, kunakuwapo sintofahamu ndani ya jamii kutokana na wengi wao kujiuliza anayejenga katika maeneo hayo.

Macha alisisitiza kuwa endapo mabango yataandikwa kwa Kiswahili itamrahisishia kila mwananchi kutambua kampuni, jina la mkandarasi, aina ya mradi kuanza kwake, kukamilika, gharama na mfadhili.

"Ninachokisema nimemaanisha, kuanzia miradi inayokuja nataka vibao viandikwe lugha ya Kiswahili ili wananchi waelewe na kuwaondolea maswali mengi dhidi ya miradi inayotekelezwa," alisema na kuongeza kuwa:

"Tukumbuke siyo watu wote wanafahamu Kingereza, mambo haya yanaleta manung'uniko mengi juu ya miradi maana watu hawaelewi kinachoendelea."

Baadhi ya wakazi wa Majengo wilayani hapa, Magdalena Mussa na Ngassa Maige, kwa nyakati tofauti waliwataka makandarasi kuacha tabia ya kuwapa kazi wazawa wa maeneo hayo na kuwachukua watu kutoka maeneo mengine.

"Kuna kazi tunazoweza kufanya wananchi wa maeneo ulipo mradi, mfano kuwapikia chakula mafundi, kusogeza vifaa vya ujenzi mawe, mchanga na maji, lakini wanapatiwa watu kutoka maeneo mengine, sisi hatunufaiki na fedha za serikali zitokanazo na miradi kupitia ajira," alisema Magdalena.

Maige, aliiomba serikali kuingilia kati suala la ajira na vibarua kwa wazawa katika miradi inayotekelezwa na serikali ili wananchi wa maeneo husika wanufaike na kuondokana na hali ngumu ya maisha.

"Sio kweli eti katika maeneo husika hawapo mafundi au vibarua wanaoweza kufanya kazi husika mpaka waletwe wa maeneo mengine, huu ni unyonyaji," alililamika.



Kambi ya madaktari bingwa 30 wa Rais Samia Suluhu Hassan wakiwa wamewasili mkoani Shinyanga tayari kwa kutoa huduma za matibabu ya kibingwa kwa wakazi wa mkoa huo juzi, ambao watatawanyika watano watano katika halmashauri zote. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Viongozi ushirika wanyooshewa kidole

**Na Timoth Itembe,** TARIME

MIGOGORO inayovikumba vyama vya ushirika nchini inadaiwa kusababisha baadhi kufa kutokana na viongozi wake kushindwa kutimiza majukumu na kujihusisha na ubadhirifu.

Madai hayo yalitolewa na baadhi ya wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Chama Kikuu cha Ushirika Mkoa wa Mara (WAMACU) wakati wa uchaguzi wajumbe wa bodi wa chama hicho.

Wajumbe hao, walisema viongozi wanaochaguliwa wanapaswa kutambua majukumu yao na kuepuka kuwaingilia watendaji wa vyama hivyo ili kukuza ushirika nchini.

Akizungumza baada ya kuchaguliwa kuwa mwenyekiti wa bodi hiyo kwa kipindi cha miaka mitatu, Momanyi Range, alisema vyama hivyo vinakufa kutokana na viongozi kuingilia utendaji wa wengine na kushindwa kudhibiti mianya ya ubadhirifu.

" Kiongozi unageuka mtendaji, mwisho wa siku mnafanya ubadhirifu kwa kushirikiana, hauwezi kuwawajibisha watendaji sababu na ni mmoja wao katika uvunjaji wa maadili, " alisema Range.

Akijivunia mafanikio ya chama hicho kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita, mwenyekiti aliyemaliza muda wake, Wamacu David Heche, alisema uwajibikaji wa bodi yake umepelekea kiwe imara.

"Tumefanikiwa kumtafuta mtendaji mkuu wa chama na kuajiri zaidi ya watu 40, tumefanikiwa kuongeza uzalishaji wa kahawa kutoka heka 2,000 hadi 3,500," alisema.

Kwa mujibu wa Heche, katika kipindi hicho, wamesambaza zaidi ya tani 20,000 za mbolea ya ruzuku kwa wakulima kwa msimu uliopita.

Alisema kwa kushirikiana na watendaji wa chama hicho, wamejenga Kiwanda cha Kahawa kwa gharama ya zaidi ya Sh. bilioni 1.3 na kupelekea wakulima kuwa na soko la zao hilo.

Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mara, Lucas Kihondere alionya serikali haitawafumbia macho viongozi wanaooua ushirika mkoani humo.

"Mwenyekiti wa bodi nakuagiza uhakikishe mafunzo yanatolewa kwa viongozi hawa wapya kuwajengea uwezo wa uelewa juu ya majukumu yao katika sekta hii muhimu kwa maendeleo ya wananchi na nchi, serikali haitakubali kurudishwa nyuma kwa masilahi ya watu binafsi," alisema Kihondere.

## Madaktari bingwa wa Samia wapiga kambi Shy

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAKAZI mkoani hapa wametakiwa kujitokeza kupata matibabu kwa madaktari Bingwa wa Kambi ya Rais Samia Suluhu Hassan ili kuboresha afya zao.

Wito huo umetolewa na Muuguzi Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Frolah Kajumla kwa niaba ya Mganga Mkuu wa Mkoa huo, Dk. Yudas Ndungile baada ya madaktari hao 30 kuwasili mjini hapa na kuanza kutoa huduma wiki iliyopita.

Florah alisema kuwa wametoa wito huo kuhasisha wananchi kuwa na mwamko wa kujitokeza kujua afya zao wakati kambi za madaktari bingwa zinapokuwa kwenye maeneo yao.

Alisema madaktari hao wamewasili Shinyanga na kuweka kambi ya siku kwa lengo la wakazi wa halmashauri sita za mkoa huo, hivyo hiyo ni fursa kwao ya kupata huduma za matibabu ya kibingwa na kuimarisha afya zao.

Mratibu wa Timu ya Madaktari Bingwa, Dk. Everine Maziku, alisema madaktari hao 30 watawafikia wakazi wote ambao watajitokeza kupatiwa matibabu.

Alisema madaktari hao wametoa huduma kwa zaidi ya wananchi 50,000 wa mikoa 20 tangu kambi hiyo ianzishwe nchini na kuwajengea uwezo watoa huduma za afya wapatao 3,500.

"Huduma ambazo zitatolewa na madaktari hawa ni za magonjwa ya wanawake, watoto, upasuaji, njia ya mkojo, ganzi, usingizi, macho, mifupa, mionzi na magonjwa ya ndani," alisema Dk. Everine kutoka Idara ya Afya, Uzazi, Mama na Mtoto Wizara ya Afya.

Baadhi ya wakazi mkoani Shinyanga, walimshukuru Rais Samia kwa kuwajali wananchi wake kwa kuhakikisha wanaendelea kuwa na afya njema.

Walisema licha ya kuboresha huduma za afya nchini, Samia ameendelea kuwapelekea wananchi madaktari bingwa hadi pembezoni mwa miji.



Ukurasa 12

**Ndivyo kuhama ovyo wafugaji kunavyovuruga maendeleo elimu**



Ukurasa 13

Nchimbi: Msiposhughulikia kero hizi mnapunguza kasi ya maendeleo


# siasa

JUMATANO JUNI 19, 2024

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU




Ukurasa 14

**ROSE MKONYI**

**Anayekosoa maelezo mwanamke katoka ubavuni mwa mwanaume**

# INEC: Watanzania milioni 35 kupiga kura mwakani

• Kujiandikisha, kuboresha kunaanzia Kigoma Julai

**Na Sabato Kasika**




Mwenyekiti wa INEC, Jaji Jacobs Mwambegele (kushoto) akiteta jambo na Mkurugenzi wa Uchaguzi wa INEC, Dk. Ramadhan Kailima. **PICHA: SABATO KASIKA**

ZIMEBAKIA takribani siku 10, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC), kuanza kuboresha daftari la kudumu la wapigakura, kazi inayoanza Julai mosi, 2024 mkoani Kigoma, mbiu inayomwamsha kila Mtanzania mwenye sifa za kuchagua viongozi wa kisiasa kujiandaa.

Uboreshaji wa daftari la wapigakura unatarajia wapigakura 34,746,638 watashiriki kuchagua rais, wabunge na madiwani katika uchaguzi utakaofanyika mwakani, anasema Mkurugenzi wa Uchaguzi wa INEC, Dk. Ramadhan Kailima.

Anasema idadi hiyo itapatikana baada ya kumalizika zoezi la kuboresha daftari hilo, akiwaambia waandishi wa habari katika mkutano wa INEC na wadau mbalimbali wa masuala ya uchaguzi, unaofanyika jijini Dar -es- Salaam.

Mkurugenzi Kailima anasema, wapigakura wapya 5,586,433 wanatarajiwa kuandikishwa na kwamba hao ni sawa na asilimia 18.7 ya wapigakura 29,754, 699 waliopo kwenye daftari la baada ya kuliboresha mwaka 2019/20," anasema Dk. Kailima.

Anafafanua kuwa katika zoezi hilo la uboreshaji wa daftari, wapigakura 4,369,531 wanatarajiwa kuboresha taarifa zao na kwamba wapigakura 594,494, wanatarajiwa kuondolewa kwenye daftari hilo.

"Hivyo, baada ya kuliboresha, inatarajiwa kuwa daftari litakuwa na jumla ya wapigakura 34, 746, 638. Tumejiandaa kutumia vituo vya 40,126 vya kuandikisha wapigakura na kuboresha daftari," anasema.

Anafafanua kuwa idadi ya wapigakura inaweza kuongezeka, kwa maelezo kwamba wapo wapya watakaofikia miaka 18 wakati wa kupiga kura, wengine ni wale ambao wakati wa kuboresha daftari mwaka 2019/20 walikuwa na sifa lakini kutokana na sababu mbalimbali hawakujiandikisha.

Aidha, Dk. Kailima anataja kuwa kutakuwa na vituo 39,709 Tanzania Bara na 417 vipo Zanzibar, na kwamba hilo ni ongezeko la vituo 2, 312 ikilinganishwa na vituo 37,814 vilivyotumika mwaka 2019/20.

Mkurugenzi wa Uchaguzi anasema, watakuwa wanatumia siku saba kwa kila mkoa kwa ajili ya kuboresha daftari hilo na kwamba wanatarajia kukamilisha kazi hiyo mwanzoni mwa 2025.

**KUBORESHA MIFUMO**

Mkurugenzi wa uandishi anasema, mfumo wa kuandikisha wapigakura kwenye daftari (Voters Registration System (VRS), umefanyiwa usanifu na kuboreshwa ili kukidhi aina ya 'BVR Kits' za sasa zinazotumia programu endeshi iitwayo android zenye uzito wa kilo 18, na kwamba ni rahisi kubebeka tofauti na za zamani zilizokuwa na kilo 35.

"Hii ni tofauti na BVR Kits za awali ambazo zilikuwa zinatumia programu endeshi ya windows zikiwa na uzito mkubwa," anasema.

Anafafanua kuwa kupitia vifaa hivyo vya uandikishaji, mpigakura anayerekebisha taarifa zake kwa njia ya mfumo huo, sharti awe na namba ya utambulisho wa taifa NIDA kwa kuwa mfumo umeunganishwa ili kuwa na taarifa sahihi za mhusika.

"Mambo ya kuepukwa wakati wa uboreshaji wa daftari ni kutoa taarifa za uongo kuhusu wewe mwenyewe au mtu mwingine ili aandikishwe kupigakura," anaeleza.

Anataja mambo mengine ya kuepukwa kuwa ni kuomba kuandikishwa zaidi ya mara ya moja, kutoa tamko la uongo kuhusu kupotea au kuharibika kwa kadi ya mpigakura au kifo.

"Lingine ni kununua au kuuza kadi ya mpigakura na kuiba au kuharibu ya mpigakura. Sisi kumbukumbu zote za mpigakura tutazipata NIDA," anasema.

**NGUVU YA KALAMU**

Mwenyekiti wa INEC, Jaji Jacobs Mwambegele, anasema, katika nchi yoyote, waandishi wa habari ndio msingi wa kwanza katika kutoa taarifa sahihi zilizofanyiwa utafiti na kuhakikiwa.

"Maana yake ni kwamba, kila kinachotolewa na INEC, hakiwezi kuwafikia wananchi iwapo vyombo vya habari havitaamua jambo hilo lifanikiwe," anasema Jaji Mwambegele.

Anaongeza: "Ni kweli tunazungumza kuwa vyama ndiyo wadau wakubwa katika zoezi hili, lakini hata wao wanatarajia vyombo vya habari kutoa taarifa."

Mwenyekiti huyo anasema, nguvu ya vyombo vya habari ndiyo msingi wa kufanikiwa kwa zoezi hilo muhimu, na kwamba waandishi wanatakiwa kutumia nafasi na fursa walizonazo kuelezea kinachoendelea katika zoezi la uboreshaji wa daftari.

"Mnaweza kutumia maneno, 'kujiandikisha kuwa mpigakura ni msingi wa uchaguzi bora, jiandikishe sasa'. Maneno haya yanaweza kuweka juu ya ukurasa wa mbele wa magazeti, juu au chini TV Kila anayetazama TV ayaone," anasema.

Aidha, ufafanuzi na ufasaha wa kuhamasisha watu kujitokeza katika zoezi hilo, hatuwezi kufanyika kwa ufanisi ila kupitia vyombo vya habari.

"Vyombo vya habari ndivyo vinaweza kuwa na sauti ya kwanza ya kuonyesha upotoshwaji wa aina yoyote inayofanywa kwa bahati mbaya au makusudi ama kwa kutojua kusema kabla ya INEC haijatoa ufafanuzi kuhusu suala lolote lililopotoshwa," anasema.

Jaji Mwambegele anasema, INEC Iko tayari kutoa ufafanuzi wa aina yoyote utakaohitajiwa na chombo chochote cha habari.

"Vyombo vya habari ndio chachu ya kufanikisha uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura. Tunategemea kuhamasisha wananchi na tunatarajia vikiendeleza kutoa habari zinazowahimiza watu kushiriki uchaguzi na waone umuhimu wa kujitokeza kujiandikisha au kuboresha ama kuhakiki taarifa zao ili kujiandaa kuchagua viongozi," anasema.

# Ndivyo kuhama ovyo wafugaji kunavyovuruga maendeleo elimu

• Ni chanzo kuacha kusoma, ndoa na mimba utotoni



Wasichana wanatakiwa kuwa darasani kusoma badala ya kuathirika kutokana na wazazi na walezi kuhama kusaka malisho. **PICHA: MTANDAO**

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

BUNGE la Bajeti linaendelea Dodoma na mojawapo ya mambo yanayokera wananchi ni migogoro ya ardhi na uhaba wa nyanda za malisho kwa ajili ya mifugo.

Tatizo la kukosa nyanda za kulishia mifugo linawapeleka wafugaji kuvamia mashamba ya wakulima, pia hifadhi za taifa lakini zinakwamisha elimu.

Ikiwa ni maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika, kukosekana nyanda hizo, kunasababisha wanafunzi kutosoma kwa vile familia zao zinahama kutafuta malisho ya wanyama.

Uchunguzi wa Nipashe unabaini kuwa, juhudi zaidi zinahitaji kupata nyanda za kutosha, ili kukabiliana na mazoea ya wafugaji kuhama kiholela kwenda maeneo mengine kutafuta malisho.

Kuhama huko kumechangia kuporomosha maendeleo ya elimu ya watoto wa mikoa ya wafugaji kama Shinyanga, Tabora, Mwanza, Simiyu na Manyara na pia kuwavurugia wasichana hatima zao.

Mtindo huo, mathalani kutoka Shinyanga kwenda Pwani au Mbeya kunalazimisha wanaosoma kuachishwa masomo na kushindwa kuendelea na shule wanapofika makao mapya.

> Wanaoingizwa kwenye ndoa ni mpango wa wazazi na walezi wanaotaka kuongeza idadi ya mifugo hasa ng'ombe pamoja na kujipatia fedha za mahari.

Kwa mfano, tatizo hili linaripotiwa kwenye Kijiji cha Ngh'omango wilayani Shinyanga, ambacho idadi kubwa ya wakazi wake ni wakulima na wafugaji wanaohamahama.

Uhamaji huo si kwa wakazi wa Ngh'omango pekee bali pia katika mikoa mingine ya wafugaji ambao wanaondoka wanapokosa malisho, bila ya kujali watoto wanaosoma iwe msingi au sekondari.

Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009, inawataka kuwapatia watoto mahitaji ya msingi kama vile chakula, malazi, mavazi, chanjo pamoja na elimu, lakini kwa upande wa wafugaji hukiuka haki hiyo.

Aidha, kifungu namba 35 cha Sheria ya Elimu ya 1978 kinaelekeza kuwa kila mwanafunzi aliyeandikishwa shule ni lazima kuhudhuria na kumaliza masomo kwa ngazi iliyosajiliwa.

Vilevile, athari za kuhama na kuacha masomo zinazungumziwa na Mwalimu Mkuu Msaidizi wa Shule ya Msingi Ngh'omango Peter Yuga, anayeeleza kuwa wazazi kuhama na watoto kusaka malisho ya mifugo kunaiathiri shule hiyo.

Yuda anasema, linapokuja suala la kuhama hawajali mambo ya elimu wala kujua wanafunzi wengine wapo kwenye madarasa ya mtihani, wanachotazama na kuthamini ni mifugo pekee si haki ya mtoto kusoma.

"Mwaka jana watoto zaidi ya 10 walihama, akiwamo na mwanafunzi wa darasa la nne ambalo wanafanya mtihani wa taifa, tulifanya jitihada za kumsaka na viongozi wa serikali, tukafanikiwa kumrudisha, akafanya mtihani na sasa yupo darasa la tano," anasema Yuga.

Anawashauri wazazi na walezi ambao ni wafugaji, wanapohama kwenda kutafuta malisho katika mikoa mingine, waangalie uwezekano wa kuacha familia zao ikiwezekana watu wachache wahame na wengine wabaki ili watoto wao wapate fursa ya kuendelea na masomo hasa wa madarasa ya mtihani na siyo kuwaachisha shule, bila kujali kuwa ni sheria, haki na serikali inagharamia elimu.

Mtendaji wa Kijiji cha Ngh'omango Madilya Nyema, akizungumzia tabia hiyo, anasema wafugaji kijijini humo wanahama kiholela wakiwa na wanafunzi, na kubainisha kuwa mwaka jana hali ilikuwa mbaya zaidi, kutokana na wafugaji kuambiwa wahame katika eneo la hifadhi ya Msitu wa Nindo.

Anasema kijiji kipo karibu na hifadhi hiyo na wananchi wengi ni wafugaji, na mara nyingi wamekuwa wakihama kiholela kwenda kutafuta malisho sehemu nyingine kuepusha ugovi na mamlaka za uhjifadhi.

Kijiji cha Ngh'omango ni miongoni mwa vijiji sita wilayani Shinyanga, ambavyo baadhi ya maeneo yao yapo ndani ya hifadhi ya Msitu wa Nindo. Vingine ni vijiji vya Mwabundala, Lyamidati, Kadoto, Mwajiji na Buzinza.

Mwaka jana Wakala wa Huduma ya Misitu (TFS) Kanda ya Magharibi, kwa mujibu wa Mhifadhi Mkuu Daraja la Pili, Lucas Nyambala, vijiji hivyo sita vilivamia eneo la msitu, lakini serikali ikaona si vyema kulichukua lote, na kuwatengea wananchi hekta 3,726 kwa ajili ya makazi, na nyingine 7,243 zibaki kwa ajili ya hifadhi.

Wananchi wa vijiji hivyo sita kikiwamo Kijiji cha Ngh'omango, wanadai kwamba eneo ambalo wamepewa kwa ajili ya makazi hekta 3,726 ni dogo mno, na hivyo wengine hasa wafugaji wameamua kuhama pamoja na watoto wao, ili kwenda kutafuta maeneo ya malisho na makazi bila kujali kuwa ni kuwaachisha masomo bila kujali hatima yao.

Lazaro Masanyiwa ni mmoja wa kazi wa kijiji hicho cha Ngh'omango, anayesema kwamba mfugaji siku zote ni mtu wa kuhamahama hana makazi maalumu, sababu ya kutafuta maeneo ya malisho ya mifugo.

Anaishauri serikali ili kulinda haki za watoto wa wafugaji kupata elimu, ni vyema Bunge likatunge sheria, uandaliwe utaratibu kuwawezesha wanakohamia wapokelewe na watoto wasime au yaandaliwe mazingira kule wanakoondoka wanafunzi wabaki kusoma.

Mwananchi mwingine Malambi Madoto, anasema watoto wengi wa wafugaji wamekuwa wakiishia njiani kimasomo, na hata wakihama huko wanapokwenda idadi kubwa hawaendelei na masomo badala yake wanaishia kuwa wachunga mifugo na wakike kuozesha ndoa za utotoni au kupata mimba.

Wanaoingizwa kwenye ndoa ni mpango wa wazazi na walezi wanaotaka kuongeza idadi ya mifugo hasa ngombe pamoja na kujipatia fedha za mahari.

Mwanafunzi Raphael Maliki kutoka shule ya Msingi Ngh'omango, anaiomba serikali kuja na utaratibu wa kudhibiti tabia hiyo ya wafugaji kuhama kiholela na wanafunzi, ili walazimishwe kuwaacha wasome na kutimiza ndoto zao.

Mratibu wa mpango mkakati wa kitaifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto (MTAKUWWA) wilayani Shinyanga Aisha Omary, anasema wamekuwa wakitoa elimu kwa wafugaji kuacha kuhama na wanafunzi, lakini wamekuwa wagumu kuelewa na wengine huhama nyakati za usiku na wanapokwenda hapajulikani na hivyo inakuwa vigumu kuwapata na hata kuwafuatilia.

# Nchimbi: Msiposhughulikia kero hizi mnapunguza kasi ya maendeleo

Na Romana Mallya



Katibu Mkuu CCM, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, akisikiliza kero za wana Usa River, Arusha. **PICHA: ROMANA MALYA**

MCHAKAMCHAKA wa ziara ya Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Emmanuel Nchimbi, mikoani umewaachia viongozi wa serikali maagizo ya kuwajibika kutatua kero za wananchi, akionya zisiposhughulikiwa zinapunguza kasi ya maendeleo.

Balozi Nchimbi akiambatana na Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo CCM Taifa, Amos Makalla na Katibu wa NEC, Siasa na Uhusiano wa Kimataifa (SUKI), Rabia Abdallah Hamid, wanazuru mikoa ya Singida, Manyara, Arusha, Kilimanjaro na Tanga.

Ziara hiyo ikianza Mei 29 mkoani Singida na kukamilika Juni 8 mkoani Tanga, anawataka kufanya kazi ya kuhudumia umma.

Somo lake kwa Watanzania na wanachama wa vyama vyote, ni kutaka kero mbalimbali za wananchi zitatuliwe kupitia maelekezo ya katibu mkuu kwa mawaziri na watendaji wengine serikalini aliokuwa akiwapigia simu.

Lengo la ziara hiyo likiwa kufuatilia utekelekezaji wa Ilani ya Uchaguzi, kuangalia maandalizi ya uchaguzi ujao wa serikali za mitaa na mkuu, kuangalia uhai wa chama na kusikiliza kero mbalimbali za wananchi.

Viongozi hao walitumia muda mwingi kusikiliza kero za wananchi zilizoibuka katika mikutano mbali mbali ya hadhara iliyofanyika kila mkoa na kuzipatia majibu nyingi zikijikita katika migogoro ya ardhi, maji, elimu, afya, masoko na baadhi wakipeleka za kuvunjia ndoa.

Katika kila mkoa, Katibu Mkuu Nchimbi anapozungumza na wananchi msisitizo wake ukawa umuhimu wa kulinda amani, mshikamano kwa kuzingatia mwaka huu, Tanzania inafanya uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu mwakani.

Akasisitiza hoja hiyo mara kadhaa kwa watu kukataa mbegu ya kuligawa taifa kwa msingi wa ukabila, udini na ukanda.

### KATAENI RUSHWA

Akiwa mkoani Singida Balozi Nchimbi, anasisitiza viongozi wakatae kutumika kwa kupewa fedha bali wazingatie kuwapima wagombea kwa uwezo wao na siyo vinginevyo.

Akataka wapimwe kwa uwezo wa kuongoza, kuheshimu watu na kubwa wanaojua matatizo ya wananchi.

Akagusia uimara wa Rais Samia Suluhu Hassan, katika nafasi ya uongozi, akisema amethibitisha kuwa nafasi hiyo ameimudu kwa kuwa mlezi wa Watanzania bila kujali itikadi zao na anahangaika wana CCM na wapinzani akiwalea wote pamoja.

Katika kuongeza msisitizo Katibu Itikadi, Uenezi na Mafunzo Makalla, anawakumbusha viongozi wasiwe mabingwa wa kusikiliza, bali kutoa majawabu ya kero wananchi wanazowapelekea.

"Utanzania ni jambo la kujisifia," ni kauli ya Katibu wa NEC, Siasa na Uhusiano wa Kimataifa (SUKI), Rabia anayesema:

"Tanzania hatuna tabia ya kushindwa, ni jambo la kujisifia na la mfano kuona tuna Rais mwanamke, nchi nyingi wamejaribu wameshindwa na sisi tutaweza tena, mwaka 2025 itakuwa ni kwa uamuzi wa Watanzania. Jamani tutunze Muungano wetu."

Akizungumza na wananchi eneo la Itaja, Singida, Balozi Nchimbi, anampigia simu, Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, kumweleza changamoto ya soko la mazao na kumtaka itatuliwe kabla ya uchaguzi mkuu, Waziri akiahidi kupeleka wataalamu haraka.

Kero nyingine inayotolewa na Mbunge wa Singida Kaskazini, Ramadhan Ighondo, ni ya mradi wa umwagiliaji Msangi ambao nao Waziri Bashe, anaahidi kuwa mipango inakwenda vizuri na una thamani ya zaidi ya bilioni 10.

Anaeleza kuwa mkandarasi ameshapatikana na kuahidi kukamilika kabla ya uchaguzi mkuu wa 2025.

Waziri huyo anawaeleza wananchi kwamba, mipango ya serikali katika kunusuru wakulima wa alizeti ni pamoja na kuweka kodi katika mafuta ya kula yanayoagizwa kutoka nje.

### CCM ITAVUKA 2025

Akiwa mkoani Manyara, Waziri Mkuu mstaafu, Frederick Sumaye, anaungana na viongozi hao katika mkutano wa hadhara wilayani Hanang, akisema chama hicho kitavuka uchaguzi mkuu mwakani, kutokana na timu imara na kazi kubwa inayofanyika .

Anasema timu ya viongozi ambayo Rais Samia ameipanga ndani ya CCM akiwamo Katibu Mkuu, Balozi Nchimbi, ni ya kuivusha CCM.

Mkoani humo viongozi hao wakatimiza agizo la Rais Samia la kutembelea nyumba za waathirika wa tope la Hanang ambazo zinaendelea kujengwa na kuwaeleza kuwa wameridhishwa na ujenzi na muda si mrefu watakabidhiwa.

Katika mkutano wake mjini Babati, Balozi Nchimbi anawaonya watendaji wanaotafuta kupewa rushwa kupitia fedha ambazo Rais Samia amekuwa akizisaka ndani na nje ya nchi kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania, kuacha mazoea hayo.

Anawataka kuona matunda ya kazi ambayo Rais Samia anafanya kwa ajili ya taifa, huku Makalla akiwaonya kuwa kinachowafanya kutembea kifua mbele ni kutokana na miradi mbalimbali kuanzia ngazi ya chini kutekelezwa katika kipindi cha miaka mitatu na nusu ya Mama madarakani.

### KERO 350 ARUSHA

Timu ya viongozi wa CCM ikiwa mkoani Arusha, Balozi Nchimbi anamwagiza Mkuu wa Mkoa, Paul Makonda, kupita kata kwa kata kutatua kero za wananchi, kutokana na mkutano wake wa hadhara jijini humo kupokea kero za wananchi 350.

Miongoni mwa yaliyojitokeza jijini humo yakibainishwa na Makonda ni pamoja na Halmashauri ya Jiji hilo mwaka 2023/24, kumwomba Rais Samia zaidi ya Sh. bilioni saba na kuletewa asilimia 98, lakini zilizotumika ni milioni 500 na nyingine hazijaguswa.

Makonda akaomba kupewa miezi sita kuanzia sasa kusafisha mkoa huo kisha ahamishwe mkoa mwingine.

Jambo jingine lililoibuliwa na wananchi wakazi wa Makuyuni, jimbo la Monduli, ni ujenzi wa makazi ya askari polisi, ambalo waliahidiwa kuwa litafikishwa Wizara ya Mambo ya Ndani kwa utekelezaji.

Kero nyingine ni ile iliyotolewa na mwanafunzi wa Chuo cha Ustawi wa Jamii Tengeru, Digna Nasari, kuhusu wanafunzi kukaa miezi sita bila kupata fedha za kujikimu (bum).

Balozi Nchimbi akijibu hilo, anatoa siku 27 ndani ya mwezi huu kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, kuitatua, lakini saa chache baada ya agizo hilo kutoka wanafunzi hao wakaanza kupata fedha.

> "Tanzania hatuna tabia ya kushindwa, ni jambo la kujisifia na la mfano kuona tuna Rais mwanamke, nchi nyingi wamejaribu wameshindwa na sisi tutaweza tena, mwaka 2025 itakuwa ni kwa uamuzi wa Watanzania. Jamani tutunze Muungano wetu.

### KILIMANJARO

Yaliyojitokeza ni pamoja na tamko la Katibu Mkuu, Balozi Nchimbi, kuonya matumizi ya dawa za kulevya hususani vijana akitaka Watanzania kufanya kila linalowezekana kukabiliana na janga hilo, huku akiwageukia wauzaji kwamba, wanapanda mbegu ya uharibifu katika taifa.

Mbunge wa Vunjo (CCM), Dk. Charles Kimei, akaibua kuhusu wananchi kulalamikia mauaji ya kijana mmoja hivi karibuni yanayodaiwa kufanywa na askari wa Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro (KINAPA) wakati mwananchi huyo akikata majani.

Katika maelekezo yake Balozi Nchimbi akasema wanaunga mkono sheria zinazolinda hifadhi ya misitu, lakini wakumbuke uhai wa binadamu ni kitu cha kwanza.

"Tunaomba wajali maisha ya watu kutumia silaha nzito kwa wananchi wasio na silaha si busara, ni jambo la hovyo, ninaielekeza serikali kuhakikisha ubinadamu unatumika katika utekelezaji wa majukumu yake.

"Haya ndiyo maelekezo rasmi kwa serikali kutumia busara tunaposhughulikia kesi zinazohusu wananchi," akaelekeza Balozi Nchimbi.

Wananchi pia, wakaonesha kiu ya mikopo maalum ya halmashauri iliyoboreshwa kwa agizo la Rais Samia ambayo itatolewa kupitia benki kwa kutaka iharakishwe ili kuweza kukuza mitaji yao.

## JUKWAA LA VIONGOZI

ROSE MKONYI

# Anayekosoa maelezo mwanamke katoka ubavuni mwa mwanaume

• Wanaume kung'ang'ania uongozi, kuzuia kinamama

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

DAKTARI Rose Mkonyi, aliyekuwa mtumishi wa Jeshi la Magereza mkoani Pwani, akitumikia nafasi ya daktari mkuu, anawahamasisha wanawake kugombea nafasi za uongozi, ili pia wajikwamue kwenye utegemezi.

Ni mstaafu na ameondoka kazini kwa zaidi ya miaka 10 sasa. Katika harakati zake za kisiasa Rose ameingia kwenye kinyang'anyiro cha kugombea ubunge na udiwani bila mafanikio.

Akipitia CHADEMA amegombea mara mbili akiomba kuchaguliwa kuwa mbunge viti maalumu na pia kwa nafasi ya mbunge wa jimbo lakini hajafanikiwa popote.

Anasema hajakata tamaa kwenye kugombea nafasi pamoja na vikwazo mbalimbali anavyokumbana navyo kutoka kwenye familia na wagombea wenzake.

Anasema uongozi wa mwanamke umekuwa hafifu, mfumo dume nao umekuwa ukimkandamiza tangu akiwa mdogo, amekuwa katika hatua ambazo zinafanya maisha ya binti, msichana na hata mama kuwa duni.

Ni kutokana na kuaminiwa kuwa kazi yake kubwa ni kulea familia na anapotaka kuongoza anaulizwa nani atasimamia majukumu ya watoto nyumbani?

Anaongeza kuwa hata kwenye imani dhana ya kuaminishwa kwamba ametoka kwenye ubavu wa mwanaume ndiyo inayoendelea kumkandamiza anapotaka kuwa kiongozi.

Anasema kwa upande wa serikali bado hakujawa na mfumo madhubuti wa kuwaandaa kisheria ili kugombea, na kama serikali haitabadilisha hili mwanamama ataendelea kuwa chini.

Rose anasema vita iliyopo kwasasa ni kupinga uwepo wa viti maalumu vya madiwani na wabunge ambavyo vimekuwa vikiwadumaza wanawake na kushindwa kusimama kwenye majukwaa kuchuana na wanaume.

"Wanawake tunaweza kuwa viongozi lakini mifumo ndiyo haijakaa sawa, tunashauri ibadilishwe anapogombea mwanaume mwanamke awe mgombea mwenza kwenye uraisi, uongozi wa shirika au kampuni, bodi...

Vivyo hivyo katika jimbo au kata mwanamke na mwanaume wagombee pamoja ili wananchi waamue ni KE au ME," anashauri.

"Kwa utaratibu huo hata inapokuja kupata wabunge au madiwani wa viti maalumu wanaangaliwa wale wanaopambana kwenye majukwaa kwanza na si hawa ambao wanagombea ndani ya chama ambao hata namna ya upatikanaji wa nafasi zao wakati mwingine unaacha maswali," anafafanua Rose.



Dk.Rose Mkonyi. **PICHA: JULIETH MKIRERI**

> Katika awamu ya kwanza alijitosa viti maalumu jimbo la Kibaha Vijijini na awamu ya pili aliingia katika Kibaha Mjini, lakini kura hazikutosha.

Rose anaiomba serikali kuweka programu za kuwajengea uwezo wanawake katika masuala ya uongozi ili waweze kujitokeza wengi kugombea badala ya kuwaacha waendelee kupambania viti maalumu ambavyo vinawalemaza.

"Tunapiga debe kuingia majukwaani kupambana na viti maalumu visiwepo wanawake wapate majimbo na kata, na njia sahihi ya kutokomeza viti maalumu ambavyo hata upatikanaji wake unalalamikiwa ni wanawake kuingia jimboni," anashauri Rose.

### VIKWAZO UONGOZI

Wakati anaanza kugombea uongozi kwa nafasi ya ubunge familia ya Rose haikumuunga mkono, huku wakibaki na dhana ya kwamba hawezi kuwa kiongozi.

Anasema familia yake hawakuwa wanamwamini lakini pia hata baadhi ya taasisi hazikuwaamini wanawake kushika nyadhifa za juu.

"Ndugu wanataka kukuona umefanikiwa lakini hawakupi ushirikiano, kwangu mtu aliyenipa ushirikiano zaidi ni baba watoto wangu ambaye anaendelea kulea familia nikiwa kwenye kampeni," anasema Rose.

Rose ambaye ameshagombea nafasi ya ubunge kwa awamu mbili katika majimbo mawili tofauti ya Kibaha anasema pamoja na kukosa nafasi hiyo hajakata tamaa.

Katika awamu ya kwanza alijitosa viti maalumu jimbo la Kibaha Vijijini na awamu ya pili aliingia katika Kibaha Mjini, lakini kura hazikutosha.

Katika mapambano yake ya kuomba nafasi ya ubunge hawezi kusahau alipotakiwa kujitoa kwenye kinyang'anyiro na mgombea mwenzake kwa sababu alizokataa kuzieleza.

"Wakati watu wanaendelea kujinadi, mwenzangu mmoja tuliyekuwa tunagombea akaniambia nijitoe lakini akaahidi akishinda tutashirikiana," anakumbusha Rose.

Anafafanua kuwa aliamua kukaa pembeni na kuacha kujinadi akiomba jina la mgombea huyo kupitishwa na chama chake kupambania ubunge Jimbo la Kibaha Mjini kutokana na ukweli kwamba aliamua kuheshimu maneno ya mwanachama mwenzake, lakini si kukataa tamaa.

"Sera yangu ya kwanza nikipata nafasi ya kuchaguliwa kuwa mbunge ni kumtetea mwanamke kwenye kudai haki zake, nikiwa muathirika kwenye mambo ya kimila lengo langu ni mgombea mwanamke apate haki zake sawa na wanaume," anasisitiza.

Rose anaeleza vikwazo vinavyokwamisha mwanamke kugombea nafasi ya uongozi ni pamoja na ushirikiano mdogo kutoka kwenye familia, kukosa fedha lakini wanaume kutokuwa tayari kuachia nafasi hizo kwa wanawake.

Vikwazo vingine alivyoeleza ni pamoja na matusi anayokumbana nayo mwanamke anapoomba nafasi za uongozi huku kauli za kwamba yeye ni mlezi wa familia hatakiwi kugombea nafasi nyingine.

Hata hivyo anasema pamoja na kwamba Rais Samia Suluhu Hassan, ameingia kwa nafasi hiyo kikatiba ni kitu ambacho kinaleta hamasa kwa wanawake wengine kugombea nafasi za uongozi.

### WASEMAVYO WENGINE

Bahati Majongo ni mmoja wa wakazi wa Mailimoja Kibaha mkoa wa Pwani anayesema ili mtoto wa kike awe kiongozi ni lazima aandaliwe akiwa bado shuleni kwa kupatiwa elimu ya stadi za maisha na uongozi.

Akimzungumzia Rose Mkonyi, anasema, amekuwa ni shujaa asiyekata tamaa na mbali ya kuwania nafasi za uongozi pia amekuwa akiunganisha wanawake na kuwapa elimu ya ujasiriamali.

Mwenyekiti wa CHADEMA, Wilaya ya Kibaha, Bumija Senkondo, anasema chama hicho ni moja ya vyama vichache vya siasa ambavyo vinawaandaa na kuwawezesha wanawake kushiriki katika masuala ya siasa na uongozi.

Bumija anasema chama hicho ambacho kina sera ya wanawake ambayo imejikita kuwawezesha kushiriki kikamilifu masuala ya umma kinalenga kuwa na asilimia 50 kwa 50 katika vyombo vya maamuzi hasa mabaraza ya madiwani na bunge na imekuwa ikipendekeza uwepo wa wabunge wawili kwa kila jimbo.

Bumija anasema Rose Mkonyi ni kati ya wanachama wa chama hicho ambao wamekuwa na haki zote kama ilivyo kwa wanachama wengine.



# Madaktari bingwa Marekani, Zimbabwe wajichimbia Singida

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MADAKTARI bingwa kutoka Marekani na Zimbabwe wameweka kambi katika Kijiji cha Pohama mkoani Singida kwa ajili ya kutoa huduma za matibabu za kibingwa kwa wananchi zaidi ya 3,000.

Waziri wa zamani wa Maliasili na Utalii, Lazaro Nyalandu ambaye ni Mwenyekiti wa Shirika la Stemm kwa upande wa Afrika ambalo ndilo limewaleta madaktari hao, akizungumza juzi wa uzinduzi wa kambi hiyo, alisema watatoa huduma za matibabu kwa wananchi wanaosumbuliwa na magonjwa mbalimbali.

Alisema jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan za kusaidia Watanzania kupata huduma bora za afya ndiyo zimewavuta wadau wa maendeleo wa kimataifa kuja nchini kutoa matibabu bure kwa wananchi.

Nyalandu alisema yeye na wadau wengine wa maendeleo wataendelea kuunga mkono jitihada za Rais Samia katika kutoa misaada ya hali na mali ili kuhakikisha utoaji wa huduma mbalimbali zikiwamo za afya zinaimarika mijini na vijijini ili kuwezesha wananchi kufanya shughuli zao za kiuchumi wakiwa na afya njema.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, akizindua kambi hiyo aliwashukuru madaktari bingwa kutoka Marekani na Zimbabwe kwa kuja nchini kutoa matibabu bure ya kibingwa kwa Watanzania maeneo ya vijijini, jambo ambalo linasaidia wananchi kutosafiri umbali mrefu kwenda kufuata huduma hizo hasa kwenye hospitali za rufani.

Kadhalika, alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa jitihada alizozifanya mpaka wanafunzi watatu walionusurika katika ajali ya basi la Shule ya St. Lucky Vincent iliyotokea mkoani Arusha kwenda kupata matibabu nchini Marekani.

Alisema mahusiano mazuri yanayofanywa na Rais Samia na mataifa mengine ya nje ndiyo yanachangia kwa kiasi kikubwa kumiminika kwa misaada mbalimbali ikiwamo katika sekta ya afya.

Hivyo, aliwaomba Watanzania kuunga mkono jitihada za serikali katika uimarishaji wa huduma kwenye sekta mbalimbali na waache kumkatisha tamaa kwa sababu Rais Samia ana maono makubwa katika kuwaletea wananchi maendeleo makubwa na endelevu.

# Biteko: Serikali inaandaa 'dawa' matatizo sekta ya mifugo

**Na Gwamaka Alipipi**

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, amesema kuwa serikali imeandaa mpango wa mageuzi ya sekta ya mifugo kusaidia kupata ufumbuzi wa changamoto zinazoikabili sekta hiyo.

Alibainisha hayo juzi mkoani Pwani wakati akifunga maonyesho ya mnada wa mifugo kwa mwaka 2024.

Akiwa katika maonyesho hayo, aliitaka Wizara ya Mifugo na Uvuvi kubuni mbinu na mikakati ya kuondokana na ufugaji usio na tija na kuwezesha kufuga kisasa.

Dk. Biteko alisema: "Wizara msichoke wala msiache kuwapa elimu wafugaji wetu, lazima tukubali kuwa wamekuwa hivyo kwa miaka mingi mabadiliko lazima yatokee na lazima tujue kuwa maeneo mengi yanayohitaji ardhi yanaongezeka ikiwa ni pamoja na mifugo lakini ardhi haiongezeki."

Kadhalika, aliwataka wafugaji watambue kwamba nchi na dunia inabadilika, hivyo nao wanapaswa kwenda na wakati kabla mabadiliko hayajawabadilisha.

Pia, aliwataka wafugaji kutojiona wadhaifu, kwamba serikali imeendelea kufanya jitihada mbalimbali ili kuboresha sekta ya mifugo nchini ikiwa ni pamoja na kutenga maeneo maalum kwa ajili ya malisho ya mifugo.

Pia, aliwaasa wafugaji kuepuka kuwa na migogoro baina yao na wakulima kwa kuwa wanategemeana na migogoro hiyo inaathari kijamii na kiuchumi.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji wa Kibiashara wa Ng'ombe (TCCS), Naweed Mulla alisema wanathamini na kutambua mchango wa vijana katika kuunga mkono jitihada zinazofanywa na jumuiya yao pamoja na serikali katika kuleta mabadiliko kwenye sekta ya ufugaji nchini.

Alisema dhumuni la TCCS ni kuona vijana wengi zaidi wakiingia katika ufugaji, wakiamini katika kukuza uchumi wa vijana kupitia sekta ya mifugo.

Naye Mkurugenzi Mwendeshaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), Frank Nyabundege, alisema wataendelea kudhamini maonyesho ya wafugaji na minada ya TCCS.

Kauli mbiu ya maonesho hayo na mnada wa kimataifa wa mifugo 2024, yalibebwa na kauli mbiu "Fuga kibiashara, tujenge kesho iliyo bora" yalifunguliwa na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Alexander Mnyeti.



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dotto Biteko (wa pili kulia), akipata maelezo kutoka kwa Pir Mohammed ambaye ni Mwanachama wa Jumuiya ya Wafugaji Kibiashara Tanzania (TCCS), wakati wa maonesho ya pili ya kimataifa ya wafugaji kibiashara 2024 yaliyofanyika juzi Kibaha, mkoani Pwani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wazalishaji mafuta ya kula wapongeza uondoaji VAT

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

CHAMA cha Wasindikaji Mafuta ya Kula ya Alizeti Tanzania (TASUPA) kimesema hatua ya serikali kuondoa kodi ya ongezeko la thamani kwa mafuta ya kula kwa kutumia mazao yanayozalishwa na wakulima nchini itahamasisha uwekezaji wa viwanda vya kuongeza mazao ya kilimo.

Pia, kimepongeza hatua ya serikali kutoa mapendekezo ya kuanza kutoza ushuru wa forodha kwa mafuta ya kula yanayoagizwa kutoka nje.

Mwenyekiti wa chama hicho taifa, Ringo Iringo alibainisha hayo jana jijini hapa, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu hatua iliyopendezwa na Waziri wa Fedha, Dk. Mwingulu Nchemba wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/25.

Iringo alisema serikali kuondoa kodi ya ongezeko la thamani kwa mafuta ya kula kwa kutumia mazao yanayozalishwa na wakulima nchini itahamasisha uwekezaji wa viwanda vya kuongeza thamani ya mazao ya kilimo nchini.

Vile vile, alipongeza serikali kwa kupendekeza katika bajeti yake iliyowasilishwa kwa mwaka fedha 2024/25 kuanza kutoza ushuru wa forodha kwa mafuta ya kula yanayoingizwa toka nje kwa asilimia 25 au 35 au Dola za Marekani 250 kwa tani kwa mafuta ghafi au Dola za Marekani 500 kwa tani kwa yaliyosafishwa.

Kadhalika, alisema sekta ndogo ya mafuta imekuwa kwa kasi katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita kutokana na juhudi na afua mahususi zinazofanywa na serikali na wadau wa maendeleo.

Alisema viwanda hivyo vinauwezo wa kukamua kwa asilimia 100 jumla ya tani za ujazo 5,000 kwa siku, hivyo kuhitaji tani za ujazo 1,800,000 kwa mwaka za alizeti.

Alisema TASUPA, inauthibitishia umma kuwa ifikapo mwaka 2027 changamoto ya upatikanaji wa mafuta ya kula nchini itakuwa imeisha na kuanza kuuza nchi za nje ka kama Jamhuri ya Demokrasia ya Congo (DRC) na Comoro.

# TRA yatoa tahadhari kwa wafanyabiashara

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), imewataka wafanyabiashara na walipakodi kutekeleza wajibu wao wa kulipa kodi, ikiwamo kufuata sheria zilizowekwa ili kuepusha usumbufu, migogoro pamoja na kuzuiliwa kwa akaunti zao.

Katika taarifa iliotolewa na Kaimu Ofisa Elimu kwa Mlipakodi na Mawasiliano kwa Umma TRA, Hudson Kamoga, inaeleza kuwa TRA inayo mamlaka ya kukusanya mapato na madeni kwa njia mbalimbali kwa wahusika ikiwamo kuwaita na kuwakumbusha kutekeleza wajibu wao.

Alisema hatua ya kuzuia akaunti ni hatua ya mwisho kabisa na kwa wale ambao watakaidi sheria iliowekwa na TRA ya kulipa kodi pamoja na malimbikizo ya madeni husika.

Kamoga alifafanua kuwa hatua hiyo hufikiwa baada ya mlipakodi kuvunja sheria, kuvunja mkataba wa TRA pamoja na kukaidi wito wa mamlaka ndipo hatua nyingine huchukuliwa kwa muhusika.

Alisema hatua nyingine kwa mlipakodi anayeshindwa kulipa kodi ni kumwandikia barua ya wito kwa ajili ya kwenda kujadiliana namna ya ulipaji wa kodi husika.

Kamoga alisistiza kuwa TRA itaendelea kutekeleza wajibu wake kwa kusimamia kwa makini na ufanisi sheria zote za kodi huku ikizingatia weledi, uwajibikaji na uadilifu.

Alisema ni muhimu kutumia kwa usahihi utoaji wa risiti za kielektroniki kila wanapouza bidhaa au huduma, kwamba husaidia kutunza kumbukumbu na hufanya ukokotoaji wa kodi kuwa rahisi.

Alisema TRA itaendelea kutoa ushirikiano na kuweka mazingira rahisi ya ufanyaji wa biashara na kuepuka mianya ya uvunjifu wa maadali.



## HABARI MBEYA

# Serikali yatakiwa kutoa bei elekezi parachichi

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MBUNGE wa Njombe Mjini, Deo Mwanyika ameitaka serikali kutoa miongozo na bei elekezi ya parachichi ili kukabiliana na ukosefu wa soko na kumnusuru mkulima kupata hasara kwa kuuza kwa bei ya chini.

Mwanyika aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari mjini hapa.

Alisema kwa sasa wakulima wengi mjini humo wanakabiliwa na tatizo la ukosefu wa soko la kuuza parachichi na kujikuta wakipata hasara.

Alisema kwa mwaka huu hali imekuwa mbaya tofauti na miaka ya nyuma kutokana na umbali wa barabara hadi kufika kwenye masoko .

"Zamani walikuwa wanakatiza hapa Suez Canal kwa hiyo kidogo ilikuwa ni afadhali, sasa hivi gharama zimeongezeka na zikiongezeka msafirishaji anayepeleka matunda nje gharama zinakuwa juu kwa hiyo lazima watafute mahali pa kupunguzia bei na siku zote anayeumizwa ni mkulima," alisema Mwanyika.

Alisema kuna haja wakulima kujifunza kuyatunza matunda ili kupelekwa sokoni wakati mwafaka.

"Ni kweli kuna changamoto kubwa sana ya bei za parachichi, wananchi na wakulima wanatakiwa waelewe tupo kwenye kipindi kigumu kwa sababu parachichi ni zao ambalo linakwenda juu na chini kwenye masoko yote ni ya nje ya nchi na yakigongana msimu ndio soko linashuka," alisema Mwanyika.

Alisema wakulima wanapaswa kuwa na mbinu bora za kilimo kwa kuyachelewesha matunda yao kupeleka sokoni.

"Wataalamu wanatuambia kama parachichi imekomaa inaweza ikakaa shambani zaidi ya miezi miwili kama inaendelea kumwagiwa maji," alisema Mwanyika.

Alisema bado serikali ina wajibu wa kuhakikisha inawapa elimu wananchi na wakulima kupitia maofisa ugani kuhusiana na kilimo hicho.

"Hatuna maofisa ugani wa kutosha kwenye zao la parachichi hata mazao mengine, kila mtu anakuwa ni mjuzi, lakini serikali inatakiwa kutoa miongozo ya zao la parachichi hata bei elekezi," alisema Mwanyika.

Baadhi ya wakulima wa Halmashauri ya Mji Njombe, walisema bei ya parachichi inasuasua na kuzua kilio kwa wakulima.

"Soko halieleweki wanunuzi wananunua parachichi kilo moja kwa Sh. 200 badala ya Sh.1,000 hadi Sh.800 tuliyokuwa tukiuza mwanzo, tunaiomba serikali iingilie kati kwa sababu hatujui hatma yetu," alisema Simon Sanga.

Valelian Mtitu, alisema wanunuzi wamekuwa wakifika katika mashamba yao na kununua parachichi kwa kilo moja Sh. 200 na kusababisha baadhi ya wakulima kukata tamaa.



Akinamama wakitoka kutafuta kuni katika eneo la Chuo Kikuu cha Dar as Salaam jana, kwa ajili ya nishati ya kupikia majumbani. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mwenge wakoleza vita dhidi ya rushwa

**Na Mwandishi Wetu,** NJOMBE

JAMII mkoani hapa imetakiwa kupambana na rushwa kwa vitendo kwa kutoa taarifa ili kujenga kizazi chenye uzalendo katika utelekezaji majukumu ikiwemo miradi ya serikali.

Rai hiyo ilitolewa Kiongozi wa Mbio za Mwenge Kitaifa mwaka huu, Godfrey Mnzava baada ya kukagua klabu ya kupambana na rushwa ya Shule ya Sekondari Mpechi mjini hapa.

Mnzava, alisema jamii na watumishi wa umma wanapaswa kujenga uzalendo katika utekelezaji wa miradi ya serikali na kutoa taarifa ya vitendo viovu au viashiria vyovyote vinavyo sababisha rushwa.

"Leo hii tumeshuhudia wanafunzi hawa wakitufundisha kwa kutumia mambo ya rushwa katika jamii, niombe viongozi wa serikali na wananchi mlio jitokeza katika eneo hili tuwe mabalozi wazuri wa kutoa taarifa juu ya uwepo wa vitendo vyote viovu vyenye viashira vya rushwa katika jamii, tukifanya hivyo basi tutakuwa na jamii bora na yenye uzalendo," alisema.

Aliwataka walimu kusimamia klabu hizo shuleni ili ziweze kuleta maendeleo chanya katika jamii na kutokomeza rushwa nchini.

Akizungumzia kuhusu uchaguzi wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji unaotarajiwa kufanyika Novemba mwaka huu nchini, Mnzava, alisema elimu

inatakiwa kuendelea kutolewa kwa wananchi ili waweze kuchagua viongozi sahihi.

"Wananchi wakipata elimu itasaidia kujua ni kiongozi wa namna gani wanamtaka na watamchagua kwa sifa zile wanazoziona," alisema Mnzava.

Awali Mkuu wa Wilaya ya Njombe, Kissa Kasongwa, alisema Mwenge wa Uhuru katika Halmashauri ya Mji Njombe utapitia miradi sita yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 2.

"Shughuli ya kwanza ni ya kupamba na rushwa na ya pili uzinduzi wa wimbo wa uhamasishaji wa uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka 2024," alisema Kasongwa.

Katika halmashauri hiyo, Mwenge umezindua miradi mitatu ukiwemo wa jengo la mama na mtoto katika Hospitali ya Mji Njombe ya Kibena, vyumba vitatu vya madarasa na ofisi Shule ya Msingi Boimanda na kukagua mitatu.

## Vijana watakiwa kuchagua wenza sahihi

**Na Mwandishi Wetu,** NJOMBE

VIJANA wametakiwa kuwa na uchaguzi sahihi kabla ya kuingia kwenye ndoa ili kupunguza wimbi la ndoa kuvunjika na kusababisha ukatili kwa watoto wao.

Wito huo ulitolewa na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Njombe, Scholastika Kevela.

Scholastika ambaye pia ni Mjumbe wa Kamati ya Kupinga Ukatili wa Kijinsia Kitaifa akizungumza na vijana walioko kwenye kambi maalumu mjini hapa, alisema wakati ugomvi unaendelea kwa wanafamilia na kupelekea mgawanyo wa mali, unazaliwa ukatili kwa watoto wanaobaki.

"Wakati tunagombana na kugawana mali nusu kwa nusu hatuwaangalii watoto na ndipo ukatili unapoingia kwa kuwa mama amechukua hamsini zake na baba hamsini zake, watoto wanabaki katikati hatimaye wahuni wanaamua kushughulika na ile familia," alisema.

Baadhi ya viongozi wa kamati hiyo Mkoa wa Njombe, akiwemo Katibu wa Siasa na Uenezi CCM wa Wilaya ya Ludewa, Shukrani Kawogo, aliwaomba vijana kuwa mabalozi kwa kutoa taarifa kwenye vyombo husika wanapoona ukatili umetokea kwenye jamii.

"Tunataka kuhakikisha ushoga, ubakaji wa watoto na ulawiti hayapo kwenye mkoa wetu, tushirikiane kwa kuwa Njombe bila ukatili inawezekana, na mkiona ukatili kwenye wilaya yako toeni taarifa bila kunyamaza," alisema Kawogo.

Mmoja wa vijana hao, Chariti Mkoni aliahidi watakuwa mabalozi wa kutokomeza ukatili dhidi ya watoto mkoani Njombe

**"Wakati tunagombana na kugawana mali nusu kwa nusu hatuwaangalii watoto na ndipo ukatili unapoingia kwa kuwa mama amechukua hamsini zake na baba hamsini zake, watoto wanabaki katikati hatimaye wahuni wanaamua kushughulika na ile familia," alisema.**



## Nishati ya gesi yapunguza matumizi ya mkaa mjini, vijijini

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Harous Suleiman Saidi amesema matumizi ya mkaa kwa kaya moja moja za maeneo ya mjini na kaya zingine za vijijini yamepungua kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya nishati ya gesi.

Aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi Zanzibar wakati akijibu swali aliloulizwa na mwakilishi wa Mwanakwerekwe, Ameir Abdallah aliyetaka kujua takwimu zikoje juu ya kupungua kwa matumizi ya mkaa kwenye ngazi mbalimbali za vijiji.

Waziri huyo alisema tathmini kamilifu ya kuangalia hali halisi ya matumizi ya mkaa kwenye ngazi mbalimbali za vijijini haijafanyika kwa siku za karibuni.

Hata hivyo, alisema takwimu ziliopo za kuingiza mkaa kutoka nje ya Zanzibar za mwaka 2017 hadi 2013 hazionyeshi mabadiliko makubwa ya kiwango cha mkaa unaoingiza kwa sababu kiwango cha juu iliripotiwa mwaka 2022 ambacho ni viroba 117,984 na kiwango cha chini ni mwaka 2021 ambacho ni viroba 93,863.

"Mheshimiwa Spika, serikali ipo katika hatua ya kufanya marekebisho ya Sera ya Nishati ya Mwaka 2009 na Sera ya Misitu ya mwaka 1999, ambayo pamoja na mambo mengine itafanya mapitio matumizi ya nishati ya Zanzibar ikiwa ni pamoja na matumizi ya nishati na mkaa," alisema.

Katika hatua nyingine, Serikali ya Zanzibar imesema Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) linadaiwa na TANESCO Sh. bilioni 9.5 hadi kufikia Februari mwaka huu 2024.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Maji, Nishati na Madini, Hassan Kaduara, katika bazara hilo la wawakilishi wakati akijibu swali la mwakilishi wa Mtambwe, Dk. Muhammed Ali Suleiman aliyetaka kujua deni la ZECO kutoka TANESCO na ni upi mkakati wa shirika hilo katika kulilipa deni hilo.

Waziri huyo alisema mkakati wa shirika wa kulilipa deni hilo ni kulilipa kwa awamu kwa kadiri bajeti itakavyoruhusu.

"Mkakati wa shirika ni kupunguza deni kwa wateja ili kupunguza limbikizo kubwa la madeni yatokanayo na umeme ni kuboresha miundombinu ya umeme, ikiwamo kufunga mita zinazomtaka mteja alipie huduma kabla ya matumizi," alisema.

Alisema pia kufanya ukaguzi kwa wateja wote ili kuondoa matatizo ikiwamo kuondoa mita zilizoisha muda wa matumizi na kulinda wizi wa umeme.

# 'Upatikanaji mawasiliano ya uhakika bado tatizo Zanzibar'

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SPIKA wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Zuberi Ali Maulid, amesema bado kuna changamoto ya upatikanaji wa huduma ya mawasiliano ya uhakika kwa baadhi ya maeneo visiwani Zanzibar, licha ya kazi kubwa iliyofanywa na serikali katika sekta ya mawasiliano.

Hivyo, aliitaka wizara husika kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) kujipanga kuhakikisha wananchi wanaoishi katika visiwa vidogo Zanzibar kwa kufanya shughuli zao za kujipatia kipato wanapata mawasiliano ya uhakika.

Aliyasema hayo katika Baraza la Wawakilishi wakati akifungua semina kwa wajumbe wa baraza hilo wa Kamati ya Mawasiliano kuhusu uelewa wa mfuko huo pamoja na kazi zake.

Alisema kuna miradi mingine inayotekelezwa na UCSAF ambayo ni pamoja na kufikisha vifaa vya TEHAMA shuleni ambapo mradi huo unahitaji kuungwa mkono kwa sababu manufaa yake ni mengi.

"Ni vyema katika miradi hii kushirikiana na wadau wengine wa maendeleo kuhakikisha kwamba shule nyingi zinafikiwa ili kujenga msingi wa matumizi ya TEHAMA kutoka katika ngazi ya shule ya msingi hadi vyuo vikuu," alisema.

Aidha, alisema mahitaji ya nchi ni mengi hivyo aliwataka viongozi wa mfuko huo kuwafikiria wanafunzi wa shule zilizopo pembezoni mwa visiwa hivyo.

Alisema ni vyema wanapopanga programu zao kuhakikisha inasura mbili kwa Unguja na Pemba ili kuweka usawa na manufaa kwa wananchi wote.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Mawasiliano ya Teknolojia ya Habari Tanzania Bara, Mohamed Khamis Abdulla alisema mfuko umefanikiwa kufikisha huduma za mawasiliano vijijini kwa upande wa Zanzibar, ikiwamo kujenga minara 42 ya simu na hivyo kuongeza usikivu wa huduma za simu.

Alisema huduma za simu kwa upande wa Unguja zimefika kwa asilimia 98 wakati kwa upande wa Pemba huduma hizo zimefikia asilimia 90.8.

Mkurugenzi Mtendaji wa UCSAF, Yustin Mashimba, alisema wapo katika hatua za mwisho kuziunganisha hospitali kuu za rufani kwa upande wa Zanzibar, ikiwamo Mnazi Mmoja na Abdalla Mzee iliyopo Pemba pamoja na hospitali nyingine za rufani ziliopo Tanzania Bara katika utoaji wa huduma za matibabu.

Alisema hatua hiyo kwa kiasi kikubwa itaongeza upatikanaji wa huduma za mawasiliano kwa madaktari katika hospitali za rufani katika utoaji wa tiba.




Mwakilishi wa Jimbo la Mwera, Mihayo Juma Nunga (kulia), akizungumza na Mwakilishi wa Jimbo la Mfenesini, Machano Othman Said katika ukumbi wa Baraza la Wawakilishi Chukwani nje ya mji wa Zanzibar. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwongozo kuwapata wajumbe bodi ya mashirika kuandaliwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MSAJILI wa Hazina Zanzibar, Wahid Muhammad Sanya, amesema ofisi yake imeandaa mwongozo mpya utakaowezesha kupatikana kwa wajumbe wa bodi za mashirika na taasisi za uwekezaji, ili kuepuka taasisi kuwa na wajumbe wasio na sifa.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari, visiwani Zanzibar katika ukumbi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Maji na Nishati Zanzibar (ZURA).

Msajili huyo alisema mwongozo huo utawezesha kuwa na wajumbe wenye sifa na uwezo wa kiutendaji kwenye bodi za mashirika ya taassi hizo.

Alisema katika utaratibu mpya wa upatikanaji wa wajumbe wa bodi kwa mashirika na taasisi hizo, utalazimisha wizara kutoa mapendekezo ya majina ya majumbe na baadaye majina hayo yafikishwe wenye Ofisi ya Msajili wa Hazina, ili kuangaliwa kama waliochaguliwa wanasifa na vigezo.

Alisema baada ya kupitia majina hayo watayarejesha kwa waziri husika, ili awatangaze na kama itatokeza kuwapo watu ambao hakidhi vigezo vilivyowekwa kisheria wataondolewa kabla ya kuidhinishwa.

Alisema utekelezaji wa jukumu hilo unatokana na Sheria ya Msajili wa Hazina ambayo inazilazimisha wizara zinapotaka kufanya uteuzi wa wajumbe wa bodi, lazima majina yao yapitie kwa msajili.

Aidha, alisema mwongozo huo utawezesha kuyafanya mashirika ya umma kujiendesha, kutengeneza faida na hatimaye kutoa gawio serikalini.

Sanya alisema kwa mujibu wa sheria inatoa mamlaka kwa Mamlaka ya Msajili wa Hazina kufanya tathmini ya utendaji kwa wajumbe walioteuliwa baada ya kuanza kazi, ikiwa pamoja na kupendekeza kwa waziri juu ya kuwaondoa kwa kuivunja bodi hiyo na kufanya uteuzi mwingine.

Akitoa mfano katika kuifanya kazi hiyo, tayari hivi karibuni ofisi hiyo ilitoa mapendekezo ya kuondolewa kwa baadhi ya wajumbe wa bodi ya Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ).

Alisema mfumo huo utaondoa mtindo uliopo kwa baadhi ya wajumbe wanaoteuliwa katika bodi za mashirika na taasisi za uwekezaji kupatikana kwa watu kusaidiana bila kuangalia vigezo vya msingi kitaaluma jambo ambalo likiisababishia mashirika kutofanya vizuri.

Akitaja mambo mengine ndani ya mwongozo huo alisema ni kuweka ukomo wa wajumbe wa bodi uteuzi wao wa kulitumikia shirika ama taasisi, kwani wamebaini wapo baadhi yao hudumu kwa muda mrefu, huku kukiwa hakuna ufanisi unaopatikana.

Alisema mwongozo huo tayari umeshamaliza maandalizi yake na umeshaanza kazi na hivi sasa wanaendelea kumalizia miongozo mingine ya kanuni za ofisi hiyo.

Akiitaja miongozo hiyo, umo wa uondoshaji wa mali za serikali, usimamizi na udhibiti wa vyombo vya moto vya serikali, mwongozo wa ukaguzi mali za serikali ambayo tayari kanuni zake zimekamilika.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTELEWA NYARAKA UMILIKI KIWANJA

**JOHN MDITI BUNANGO** anatangaza kupotelewa na nyaraka umiliki wa kiwanja namba 878 Kitalu"DD" kilichopo Lubaga Manispaa ya Shinyanga Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na John kwa simu namba **0754-654840**

**TAARIFA YA POLISI: PHQ/SHI/SHI/4509/2024**

## KUPOTEA KWA PIKIPIKI

**RAMADHANI RASHIDI HASSAN** anatangaza kupotea kwa pikipiki aina ya **PULSAR** yenye usajili namba **MC 294 BHJ, CHASSIS NAMBA: MD2DHJZZUCG83489** na **ENGINE NAMBA: IM4204**.Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/KIN/118871/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**NICHOLAUS NJAU** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.0341/0221 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia SANGU HIGH SCHOOL mwaka 2005. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/UBU/116531/2024**

**IN THE DISTRICT MAGISTRATE COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 13991 OF 2024**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE GODWIN HERMAN SHEMBILU**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATIONFOR LETTERS OF ADMINISTRATION**
**BY HELIME SINGANO**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75of Probate Rules GN 369 of 1963)**

ALL PERSONS Claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Admirations ismade to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 17 Day of July 2024.

Date at Dodoma this 14thday of June 2024


..................................................

**PETITIONER**

..................................................

**PRINCIPAL /SENIOR/RESIDENT MAGISTRATE**

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**SALIM AHMED MKANGA** ANATANGAZA KUPOTEA KWA PASSPORT YAKE YENYE NO TAE 246009 ILIYOTOLEWA TAREHE 25 NOV 19 NA IDARA YA UHAMIAJI DAR -ES -SALAAM.

KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ANAOMBWA KUIPELEKA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU

**TAARIFA :PHQ/KIL/MOS/4381/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ABADI MAULID ALLY** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajiri **T. 444 DRF** aina ya **TOYOTA LAND CRUISER.**

Yeyote atayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake.

Taarifa ya polisi;

**PHQ/SHI/KAH/4331/202**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**MAHALI DODOMA**
**MAOMBI NA. 108 MWAKA 2024**
**BAINA YA**
**TADEI SELESTINI TARIMO...............MDAI**
**DHIDI YA**
**ROBERT SAIMON TARIMO................MDAIWA**
**WITO/KUITWA SHAURINI**

**KWA**
**ROBERT SAIMON TARIMO**
**POPOTE ULIPO.**
**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya Maombi amabayo inapatikana katika Baraza hili.

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi , Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 11/07/2024 saa 3:00 kamili Asubuhi kwa ajili ya kutaja .

ANGALIZO:

Kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likithibitisha kuwa umepokea Hati ya Wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 07 ya Mwezi Juni, 2024.

.....................................

**MWENYEKITI**
**Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**JOHNSON KAROKORA KARAZE**

ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI AINA YA KINGLION NYEUSI YENYE USAJILI NO. MC 583 CZJ, CHASSIS NO.LZL15P90IMF50359, ENGNE NO. KL162 FMJ 210650359. TAARIFA YA POLISI

**PHQ/MWA/NYA/1939/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**SHADRACK ANDREA MAGANGA**

ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI MC 553 AQW, AINA YA PIKIPIKI NI ZONGSHEN KWA YOYOTE ATAKAEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI.

TAARIFA YA POLISI:

**PHQ/MBE/MBE/295/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**VAILETH VERRY KATABARUKI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0454-0050 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia ST. JOSEPH SECONDARY SCHOOL mwaka 2020. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: PHQ/ARU/ARU/14688/2024**


# OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0677020701 E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ, WEBSITE: WWW.IPPMEDIA.COM


**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Spika Dk. Tulia ampeleka Mpina Kamati ya Maadili

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson ameagiza Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ikutane mara moja kumhoji Mbunge wa Kisesa, Luhaga Mpina (CCM).

Hiyo ni baada ya mbunge huyo kufanya mkutano na vyombo vya habari kuzungumzia maudhui ya ushahidi aliokabidhi kwa Spika wa Bunge, jambo ambalo ni kinyume cha sheria, kanuni na taratibu za Bunge.

Spika alimtaka Mpina kuwasilisha ushahidi kuhusu tuhuma zake dhidi ya Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe kudanganya Bunge.

Kiongozi huyo wa Bunge alieleleza hayo jana, akiagiza kamati hiyo ya Bunge ikutane mara moja kutafakari jambo hilo lililofanywa na Mpina na kutoa maoni na mapendekezo ya nini kifanywe na chombo hicho cha kutunga sheria.

"Kuhusu ushahidi uliowasilishwa na Mpina kuthibitisha tuhuma zake kwamba Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe amesema uongo bungeni, ninaikabidhi pia Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ushahidi wote ili kamati iupitie na kutoa maoni iwapo ushahidi huo unathibitisha tuhuma kwamba Waziri wa Kilimo amesema uongo bungeni na nini kifanywe na Bunge," alisema Dk. Tulia.

Aliagiza kamati hiyo ianze kushughulikia masuala hayo mara moja kuanzia jana na kuwasiliisha taarifa kwake siku ya Jumatatu Juni 24 mwaka huu.

"Waheshimiwa wabunge, mtakumbuka tarehe 4 Juni 2024 katika kikao cha 40 cha mkutano wa 15 wakati wa majadala wa hoja ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Fedha kwa mwaka fedha 2024/25, Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe pamoja na mambo mengine alichangia kwamba kampuni na viwanda vya sukari nchini vilivyopewa dhamana na serikali ya kuhahakikisha kunakuwa na sukari ya kutosha nchini imeshindwa kutekeleza wajibu huo.

"Wameshindwa kuagiza na kusambaza sukari kutoka nje ya nchi kama inavyotakiwa na kwamba hali hiyo imesababisha kuendelea kuwapo tatizo la uhaba wa sukari nchini.

"Aidha, waziri aliendelea kueleza kuwa jambo hilo lilisababisha bei ya sukari nchini kuendelea kupanda hadi kufikia Sh. 10,000 kwa kilo moja," alisema Dk. Tulia akimnukuu Waziri Bashe.

Spika Tulia alisema wakati waziri anaendelea kuzungumza, Mpina alipata nafasi ya kutoa taarifa kuhusu mchango wa Bashe, akionesha kuwa waziri alikuwa anadanganya Bunge kwa sababu kampuni na viwanda vilivyopewa dhamana kuagiza sukari havijashindwa kutimiza wajibu wao, bali upande wa serikali ndiyo umekuwa kikwazo cha kufanikisha lengo hilo.

Alisema katika taarifa yake, Mpina alisema serikali imeshindwa kushirikiana na wenye viwanda na kampuni zilizopewa dhamana ya kuagiza sukari na hivyo kusababisha kuadimika kwa sukari na kupanda kwa bei ya bidhaa hiyo, hivyo kuleta kadhia kwa wananchi.

"Mheshimiwa Mpina aliendelea kusisitiza kwamba waziri amedanganya Bunge na kwamba anao ushahidi kuthibitisha jinsi wizara inavyochangia kuendelea kuwa na tatizo la uhaba wa sukari nchini," alisema.



Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson akitoa taarifa yake, Bungeni jijini Dodoma jana, kuhusu Mbunge wa Kisesa, Luhaga Mpina kukiuka kanuni kwa kuzungumza na waandishi wa habari, baada ya kukabidhi ushahidi wake kwa Spika wa Bunge Juni 14 mwaka huu. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

Spika Tulia alisema kuwa baada ya taarifa hiyo ya Mpina, alitoa ufafanuzi kuhusu masharti ya kanuni ya 70 kuhusu kutosema uongo bungeni. Mbunge yeyote anayetoa tuhuma kuhusu mbunge mwingine anasema uongo bungeni, anatakiwa kuwasilisha ushahidi ili kuthibitisha uongo huo.

"Hivyo, kwa kutumia kanuni hiyo nilielekeza Mheshimiwa Mpina awasilishe ushahidi ifikapo tarehe 14, Juni 2024 ili kuthibitisha tuhuma kwamba Waziri wa Kilimo amedanganya Bunge.

"Tarehe 14, Juni 2024, Ofisi ya Bunge ilipokea barua kutoka kwa Mbunge Mpina iliyowasilisha nyaraka za ushahidi kama nilivyomwelekeza. Waheshimiwa wabunge wote, mnafahamu kanuni zetu hasa zinazoainisha utaratibu wa kushughulikia tuhuma za mbunge kusema uongo bungeni," alisema kiongozi huyo wa Bunge.

Alisema taratibu zinaelekeza mbunge yeyote aliyeko bungeni anaweza kumtaarifu Spika kwamba mbunge anayezungumza bungeni, wakati anatoa maelezo, anatoa maelezo ya uongo. Spika atatakiwa kuthibitisha ukweli kuhusu jambo hilo, uthibitisho huo utatolewa papohapo au katika muda ambao spika ataelekeza, uthibitisho utakaotolewa unatakiwa kuwa wa kiwango cha kulidhisha Bunge.

Alisema Spika anapokea ushahidi na ana mamlaka ya kupitia yeye mwenyewe na kulitaarifu Bunge. Spika pia anaweza kupeleka nyaraka zilizowasishwa kwa kamati ipitie nyaraka hizo na kuwasilisha maoni kwa Spika kuhusiana na kuthibitishwa au kutothibitishwa kwa tuhuma za mbunge kudanga Bunge. Spika akishapokea taarifa hiyo ya kamati, ataarifu Bunge.

"Kama nilivyoeleeza hapo awali, nilimwelekeza Mbunge Mpina kuwasilisha ushahidi wake kwangu ifikapo tarehe 14 Juni 2024 kwa lengo la kupima ushahidi huo dhidi ya kauli ya Waziri wa Kilimo.

"Hata hivyo, kabla sijachukua hatua yoyote kujiridhisha kuhusu ushahidi huo au kuupeleka kwenye kamati ili kamati ichambue ijiridhishe. Baada ya kuleta taarifa kwangu, Mpina aliitisha mkutano na waandishi wa habari," alisema.

Spika Tulia alisema kuwa katika mkutano huo, Mpina aliyaeleza yale ambayo alikuwa ameeleza katika nyaraka za ushahidi alizowasilisha Ofisi ya Spika.

Alisema kuwa kuanzia Juni 14, 2024, vyombo vya habari na mitandao ya kijamii vimeendelea kurusha mkutano huo wa Mpina na watu mbalimbali wameendelea kuchambua ushahidi wa nyaraka hizo zilizowasilishwa kwake na wengine kufikia hatua ya kutoa hukumu.

"Mheshimiwa Mpina amekuwa bungeni kuanzia mwaka 2005, hivyo ni mbunge mzoefu na anazifahamu ipasavyo sheria, kanuni na taratibu zinazoongoza Bunge.

"Ni dhahiri kitendo cha yeye kufikisha nyaraka za ushahidi kwa Spika na wakati huohuo kukutana na vyombo vya habari kuhusu maudhui ya nyaraka hizo ni kitendo cha utovu wa nidhamu kwa Bunge na Spika, kudharau mamlaka ya Spika, kuingilia mwenendo wa Bunge na kushusha hadhi na heshima ya Bunge," Spika Tulia alitamka kwa hisia kali.

# Tanzania kujenga majengo pacha Kenya

**Na Mwandishi Wetu,** NAIROBI

SERIKALI imezindua ujenzi wa majengo pacha ya ghorofa 22 kila moja, jijini Nairobi yatakayotumika kama Ofisi ya Ubalozi wa Tanzania nchini Kenya na kitega uchumi kwa ajili ya kuongeza fedha za kigeni nchini.

Kwa sasa, Tanzania inatumia Sh. bilioni 29 kwa mwaka kulipia kodi kwa ajili ya balozi na makazi ya watumishi wake wanaofanya kazi nje ya nchi na ujenzi huu unaelezwa kuwa ni mkakati wa Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan kutumia viwanja na majengo yake kuongeza mapato ya nchi.

Uzinduzi huo uliofanyika katika eneo la kibiashara la Upper Hill, jijini Nairobi, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba, alisema majengo hayo ambayo ujenzi wake utagharamiwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa NSSF, yataipa Tanzania fursa ya kutumia eneo la Kenya kujenga ubalozi na kupangisha kwa makazi na ofisi eneo hilo ili kupata fedha.

"Kwa sasa kwa mwaka tunatumia wastani wa shilingi bilioni 29 kulipa gharama za kupangisha ofisi zetu za kibalozi na nyumba za mabalozi wetu duniani kote. Kupitia mkakati huu mpya ambao unaanzia Kenya, tumepanga kuanza kuingiza zaidi ya shilingi bilioni 36 kwa mwaka kupitia uwekezaji tutakaofanya kwenye majengo na viwanja vyetu vilivyopo ughaibuni.

Tanzania itajenga majengo hayo kwenye eneo ililopewa bure na Serikali ya Kenya kwa ajili ya kujenga ubalozi wake - ikijibu ukarimu wa namna hiyo uliofanywa na Tanzania kwa kuipa Kenya bure eneo ambako imejenga ofisi za ubalozi wake, Oysterbay jijini Dar es Salaam.

Eneo hilo ambalo Tanzania imepewa kujenga ubalozi wake, ni mojawapo ya maeneo ya kimkakati jijini Nairobi, kukiwa na ofisi nyingi za serikali huku ikiwa inatazamana na ulipo ubalozi wa Uingereza katika taifa hilo.

Akizungumza katika tukio hilo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira, Vijana na Walemavu), Deo Ndejembi, alisema uamuzi wa kujenga majengo hayo ulizingatia upembuzi yakinifu uliofanywa na wataalamu na kuona namna mradi utakavyoingiza mapato kwa serikali.

Kwa sasa, ubalozi wa Tanzania nchini Kenya unafanya shughuli zake katika ghorofa ya tisa ya jengo la Re Insurance ambako serikali inalipa kodi ya pango kwa ubalozi na inalipia pia kodi za pango kwa watumishi wake wanaoishi nchini humo.

Mgeni rasmi katika tukio hilo, Waziri Mkuu na Waziri wa Mambo ya Nje wa Kenya, Musalia Mudavadi, alipongeza hatua ya Tanzania kujenga jengo hilo akisema litakuwa mojawapo ya alama za kudumu za uhusiano wa kirafiki baina ya nchi hizo mbili.

Mudavadi ambaye aliwahi kuwa Waziri wa Fedha wa Kenya, alisema serikali yao pia imejifunza kitu kuhusu namna ya kutumia fedha za taasisi kama NSSF kwa kufanya uwekezaji ili zizalishe zaidi na kuwa muda si mrefu, Kenya itafuata nyayo za Tanzania kwenye utaratibu huo.

Tanzania ina jumla ya majengo 109 na viwanja 11 duniani. Pia ina jumla ya balozi 45 na Konseli Kuu tano na kwa mujibu wa mkakati mpya uliopitishwa na Wizara ya Mambo ya Nje hivi karibuni, lengo la serikali ni kutaka kuona inatumia mali zake hizo kuingizia nchi mapato

# TABORA UNITED KUSUKA KIKOSI TISHIO MSIMU UJAO

**Adam Fungamwango na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kufanikiwa kubaki Ligi Kuu, Klabu ya Tabora United imeahidi kufanya usajili wa nguvu kwa ajili kukisuka upya kikosi chao ili kiwe cha ushindani msimu ujao, badala ya kunusurika kushuka kama ilivyokuwa msimu huu.

Akizungumza mwishoni mwa wiki baada ya kumalizika kwa mchezo wa 'play off' kati ya timu hiyo na Biashara United, Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mjini Tabora, ikishinda mabao 2-0, Kaimu Kocha Mkuu wa timu hiyo, Bernad Fabiano, alisema sasa watalazimika kujipanga upya kwa ajili ya kukitengeneza kikosi bora msimu ujao, kwani msimu huu hali ilikuwa ngumu.

**"Watu wameona, tumepambana sana, ila mchezo tuliuanza vibaya kwa sababu ya presha, tulikuwa nyum a, lakini baada ya kupata bao tukatulia, baadaye tukapata bao la pili.**

Wapinzani wetu walikuja na mpango mkakati wa kutaka kupata bao la mapema kwa hiyo mechi ikawa ngumu, nawashukuru mashabiki kwa kujitokeza kwa wingi kuja kutupa sapoti, mimi mwenyewe nimejiwekea rekodi ya kuipandisha hii timu, leo nimeibakisha, ingeshuka, maana yake ningeishusha mwenyewe," alisema kocha huyo ambaye amechukua mikoba ya Masoud Djuma, aliyeondolewa baada ya kichapo cha mabao 4-0 katika 'play off' ya kwanza dhidi ya JKT Tanzania.

Matokeo hayo yameifanya Tabora United kubaki Ligi Kuu kwa jumla ya mabao 2-1, kwani katika mechi ya kwanza iliyochezwa Juni 12, Uwanja wa Karume mjini Musoma, Mara, ilifungwa bao 1-0 lililowekwa wavuni na Helbert Lukindo, huku mechi ya juzi, mabao yote yakitiwa kwenye kamba na Patrick Lembo.

Kocha Mkuu wa Biashara United, Amani Josia, amesema matumizi ya nafasi ndiyo yamewagharimu.

Biashara United ilihitaji bao moja tu ili iweze kufuzu kwa bao la ugenini, lakini hali ilikuwa ni ngumu kwa vijana hao.

"Nafikiri ni matumizi ya nafasi yalitugharimu, kuna faida tulizipata kwenye mechi hii, na tulistahili penalti, lakini mwamuzi hakutupa, mechi ilikuwa nzuri, Tabora na Biashara wote tulikuwa sawa, tumekosa bao moja tu ili twende Ligi Kuu, hilo ndilo limetugharimu, lakini tumejifunza kitu," alisema.

Kwa upande wa Msemaji wa Tabora United, Christina Mwagala, aliliambia Nipashe jana kuwa wachezaji wamefanya kazi kubwa kuhakikisha wanabaki kwenye ligi hiyo.

"Ninawapongeza wachezaji wetu kutokana na juhudi waliyoionyesha katika na hatimaye msimu ujao tutakuwapo kama kawaida," alisema Mwagala.

Alisema kwa sasa wanasubiri kupokea ripoti ya benchi lao la ufundi ili kamati ya usajili ianze zoezi la usajili kwa lengo la kuiboresha zaidi timu yao.

Mwagala alisema kwa sasa wanaanza mikakati yao kuelekea msimu ujao na kudai wataendeleza ushindani ili washike nafasi ya juu kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.



Mchezaji wa timu ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Hashimu Omary (kulia), akiuwahi mpira dhidi ya wachezaji wa timu ya Chuo cha Usafirishaji (NIT), wakati wa mechi ya kirafiki iliyochezwa Uwanja wa Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam juzi na NIT kushinda mabao 2-1. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## JKT Queens kushusha nyota

**Na Shufaa Lyimo**

BENCHI la ufundi la timu ya JKT Queens, imesema linatarajia kuboresha kikosi chake kwa kufanya usajili wa kishindo ili kushika nafasi ya juu kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya Wanawake msimu ujao

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Ester Chaburuma, alisema miongoni mwa safu atakazoziboresha ni safu ya ushambuliaji na kiungo

"Safu hizo ndio ambazo zilikuwa na mapungufu msimu uliopita, hivyo ninapaswa kufanya marekebisho makubwa ili msimu ujao tushike nafasi ya juu, alisema Chaburuma ambaye kikosi chake hicho kimeupoteza ubingwa msimu huu baada ya Simba Queens kuubeba.

Alisema kwa sasa ni mapema kutaja idadi ya wachezaji atakaowaacha na atakaowasajili, na kuwataka mashabiki wao wawe watulivu kipindi hiki cha usajili.

"Kwa sasa siwezi kutaja idadi ya wachezaji nitakaowaacha na kuwasajili, ninaomba mashabiki wetu wawe wavumilivu muda ukifika nitawataarifu ili wajue kinachoendelea," alisema Kocha huyo.

## Gofu Lugalo mabingwa Morogoro Open

**Na Mwandishi Wetu**

KLABU ya Gofu Lugalo imeibuka na ushindi kwenye shindano ya Morogoro Open 2024, lililomalizika mwishoni mwa wiki kwenye Klabu ya Gofu Morogoro.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa shindano hilo, Meneja wa Klabu ya Gofu Lugalo, Kanali David Mziray, aliwapongeza wachezaji wake kutokana na juhudi walizozionyesha katika shindano hilo.

"Ninawapongeza wachezaji wangu kutokana na juhudi waliyoionyesha kwenye shindano hilo ambalo lilikuwa na ushindani mkubwa," alisema Mziray.

Aidha alisema baada ya ushindi huo kwa sasa wanajipanga kwa ajili ya mashindano mengine, na kuwataka wale walioshindwa kutokata tamaa bali wajipange upya.

# *Dodoma Jiji FC yavunja benchi lote la ufundi*

**Na Adam Fungamwango**

WIMBI la klabu kuvunja mabechi ya ufundi baada ya Ligi Kuu kumalizika limeendelea tena baada ya Dodoma Jiji kuamua kuachana benchi lake lote la ufundi, lililokuwa chini ya Mkenya, Francis Baraza.

Hii inakuja siku mbili tu baada ya JKT Tanzania nayo kuvunja benchi la ufundi lililokuwa likiongozwa na Malale Hamsini mara baada ya kumalizika kwa Ligi Kuu na mechi za 'play off'.

Katibu Mkuu wa Klabu ya Dodoma Jiji, Johnson Fourtunatus, amesema uamuzi huo umefikiwa baada ya majadiliano ya muda mrefu, pamoja na makubaliano baina ya wahusika.

"Uongozi tumefikia makubaliano ya kutomuongeza tena mkataba kocha Baraza, baada ya mkataba wa awali kumalizika, hatutaendelea naye. Na baada ya makubaliano hayo, tumeamua kuvunja benchi lote la ufundi kwa minajili ya kuboresha eneo hilo. Tunatoa shukrani za dhati kwa kocha na wasaidizi wake kwa mchango mkubwa walioutoa katika kipindi ambacho tulikuwa pamoja, na kwa sababu hiyo tunatarajia kutangaza rasmi benchi jipya la ufundi wakati wowote kuanzia sasa," alisema Katibu Mkuu huyo.

Baraza alikuwa akisaidiwa na Kassim Liogope ambao waliifikisha timu hiyo nafasi ya 12 kwenye msimamo wa Ligi Kuu, na ilisubiri hadi mechi ya mwisho kujihakikisha kubaki, ambapo kabla ya hapo ilikuwa kwenye hatihati ya kushuka au kwenda 'play off'.

JKT Tanzania, hivi majuzi ilivunja benchi la ufundi lililoongozwa na Malale ambaye alifanikiwa kuibakisha timu hiyo Ligi Kuu, baada ya kushinda mabao 4-0 katika michezo miwili ya 'play off' dhidi ya Tabora United.

Hata hivyo, mabosi wa maafande hao walionekana kutoridhishwa na timu yao kufanya vibaya hadi kuponea kwenye mechi za mchujo.

## ZISIKUPITE

### MKATABA MPYA BIGHTON

KLABU ya Bighton imeanzisha mazungumzo juu ya mkataba wa winga wa Uholanzi, Crysencio Summerville mwenye umri wa miaka 22, kutoka Leeds ***(Talksport)***

### TORRES KATIKA RADA

WINGA wa HIspania, Ferran Torres anasakwa na West Ham msimu huu wa majira ya joto, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, hataki kuondoka Barcelona. ***(Mundo Deportivo)***

### SPURS YAZUIWA KWA TONEY

OMBI la Tottenham Hotspur la kumsajili mshambuliaji wa England, Ivan Toney mwenye umri wa miaka 28, limekataliwa na Brentford. ***(Football Transfers)***

### AIVUTIA FENERBAHCE

KLABU ya Fenerbahce inavutiwa na beki wa Manchester United mwenye umri wa miaka 29 kutoka Sweden, Victor Lindelof. ***(Sky Germany)***

### GUEHI SOKONI MIL. 65

KLABU ya Crystal Palace itadai ada ya takriban pauni milioni 65 kwa mlinzi wa England, Marc Guehi mwenye umri wa mika 23, msimu huu wa majira ya joto. ***(Telegraph)***

### GALLAGHER ASAKWA

ATLETICO Madrid wanaisaka saini ya kiungo wa kati wa Chelsea, Conor Gallagher, 24. ***(Relevo)***

### WILLIAN FRESH CHELSEA

WINGA wa Brazil, Estevao Willian amefuzu vipimo vya afya ili kujiunga na Chelsea, ambayo ilikubali kumsajili kinda huyo mwenye umri wa miaka 17 kutoka Palmeiras mwezi uliopita. ***(Standard)***

### MAN CITY KUTOSAJILI

KLABU ya Manchester City ipo tayari kuingia msimu ujao bila kufanya usajili mpya isipokuwa iwapo mchezaji ataomba kuondoka. ***(ESPN)***

### ANYATIWA NEWCASTLE

NEWCASTLE United ina nia ya kumsajili winga wa Iceland, Jon Dagur Thorsteinsson mwenye umri wa miaka 25, kutoka Klabu ya OH Leuven ya Ubelgiji. ***(Chronicle Live)***


### TOMORI KUKATAA OFA

MLINZI wa AC Milan, Fikayo Tomori mwenye umri wa miaka 26, huenda akakataa ofa yoyote kutoka kwa Newcastle United msimu huu. ***(Football Insider)***

### HUMMELS KUTUA MALLORCA

BEKI wa zamani wa Ujerumani, Mats Hummels mwenye umri wa miaka 35, anakaribia kusaini mkataba wa kujiunga na Real Mallorca baada ya kuondoka Borussia Dortmund. ***(Diario de Mallorca))***

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI Y[...]A



# MBAPPE AEPUKA UPASUAJI WA PUA

## Arejea kikosini, sasa kutengenezewa mask maalum ambayo ataivaa wakati wa...

**DUSSELDORF,** Ujerumani

NYOTA wa Ufaransa, Kylian Mbappe, amepelekwa hospitalini mjini Dusseldorf baada ya kuvunjika pua katika ushindi wa bao 1-0 wa Ufaransa dhidi ya Austria kwenye michuano ya Ulaya nchini Ujerumani, juzi.

Baada ya hapo awali kuhofia kuwa mshambuliaji wao nyota angehitaji kufanyiwa upasuaji na huenda akakosa baadhi ya michuano ya Euro 2024 au yote, rais wa Shirikisho la Soka la Ufaransa, Philippe Diallo, alimwambia Julien Laurens wa ESPN kwamba madaktari wa timu hiyo waliamua kwamba Mbappe atakuwa sawa bila kufanyiwa upasuaji baada ya kufanyiwa vipimo.

**Mshambuliaji huyo wa Real Madrid aliondoka hospitalini saa moja asubuhi jana kwa saa za huko na amerejea kwenye timu.**

Mbappe atatengenezewa mask maalum ambayo atahitaji kuvaa atakaporudi kucheza katika mchezo wa Ijumaa dhidi ya Uholanzi.

Mshambuliaji huyo, aliyehusika katika bao la kipindi cha kwanza, aligongana kichwa na Kevin Danso wa Austria mwishoni mwa mchezo wa Kundi D Uwanja wa Dusseldorf Arena.

"Ameumia pua," alisema kocha Didier Deschamps.

"Itabidi tusubiri tuone, madaktari wanalishughulikia, itabidi tuone kitakachofanyika halafu itachukua muda gani, ni habari mbaya sana kwetu.

"Ni wazi, timu ya Ufaransa ikiwa naye au bila yeye, hii sio kitu sawa. Natumaini anaweza kuwa huko."

## HABARI MICHEZO

# RAMOS HURU KUTUA KLABU YOYOTE



**MADRID,** Hispania

KLABU yoyote inayohitaji saini ya beki Sergio Ramos itampata baada ya mkataba wake na Sevilla kumalizika, hivyo yupo huru.

Ramos mwenye umri wa miaka 38, alijiunga na klabu hiyo akitokea Paris Saint Germain ambako alifunga mabao manne ndani ya misimu miwili 2021-2023.

Mhispania huyo alijiunga na PSG akitokea Real Madrid ambako alijiunga 2005 akitokea Sevilla.

Taarifa za mtandao wa Sports zinaonesha Ramos alikuwa akipokea mshahara wa pauni 46,000 kwa wiki akiwa na klabu hiyo.

Hata hivyo, zipo taarifa kuwa huenda Ramos akatimkia Saudi Arabia ambako kuna baadhi ya nyota aliowahi kucheza nao akiwamo Cristiano Ronaldo na Karim Benzema.

Ramos alianza soka akiwa na Klabu ya Camas mwaka 1991 na baadaye kwenda Sevilla, mwaka 2003, kabla ya 2005 kujiunga na mabingwa wa kihistoria wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, Real Madrid.

## Simon azigonganisha Manchester Utd, Arsenal

**LONDON,** England

ARSENAL na Manchester United ni miongoni mwa klabu zinazopigania huduma ya Mholanzi, Xavi Simon anayekipiga RB Leipzig ya Ujerumani kwa mkopo.

Taarifa iliyoripotiwa na mtandao wa Sky Sport ukiunukuu mtandao wa L'Equipe imeeleza klabu hizo zimewasiliana na Paris Saint Germain ambao ndio wamiliki wa mchezaji huyo kuhusu uwezekano wa kumsajili katika dirisha hili.

Taarifa hiyo imeeleza Bayern Munchen pia imeonesha dhamira ya kutaka saini ya kiungo huyo wa pembeni, licha ya ripoti kuwa PSG hawana mpango wa kumuuza.

Sky Sport wameripoti kuwa PSG inapanga kubaki na nyota wao, hata hivyo wana mpango wa kumtoa tena kwa mkopo kwa msimu mwingine.

Akiwa na RB Leipzig kwa mkopo, Simons alifunga mabao 10 na kutoa pasi za mabao 15 msimu uliopita.

Miaka kadhaa nyuma akiwa PSV ya Uholanzi, Arsenal iliwahi kuhusishwa kutaka saini ya mchezaji huyo ambaye kwa sasa yupo katika majukumu ya timu ya taifa kwenye mashindano ya Euro2024.





## *Boston Celtics yaweka rekodi ya ubingwa*

**BOSTON,** Marekani

TIMU ya Boston Celtics imetwaa taji la Ligi ya Mpira wa Kikapu nchini Marekani msimu wa 2023/2024 baada ya kuitandika Dallas Mavericks kwa vikapu 106-88 katika mchezo wa awamu ya tano.

Ubingwa huu ni rekodi kwa timu hiyo ikiwa ni mara ya 18 kufanya hivyo, mara nyingi zaidi kuliko timu nyingine yoyote ikifuatiwa na Los Angeles Lakers iliyobeba mara 17.

Ushindi huo ulichangiwa na viwango bora vya wachezaji kama Jayson Tatum aliyefunga vikapu 31, 'rebounds' nane na kutoa pasi 11 zilizozalisha vikapu. Jrue Holiday alimaliza mchezo akiwa na vikapu 15 pamoja na rebounds 11.

Jaylen Brown amechaguliwa kama Mchezaji Bora wa michezo ya Fainali (FINALS MVP) na katika mchezo huu alimaliza akiwa na vikapu 21.

Rekodi nyingine iliwekwa na kocha Joe Mazulla mwenye miaka 35 ambaye amekuwa kocha mwenye umri mdogo zaidi kutwaa ubingwa wa NBA tangu Bill Russel mnamo mwaka 1969.

HABARI MICHEZO

## Msuva afungua milango Yanga

INATOKA UKURASA 24

adhabu ya kufungiwa kusajili," ilieleza sehemu ya taarifa hiyo.

TFF imesema mpaka jana asubuhi, hakuna klabu yoyote kati ya hizo iliyowalipa wahusika, ikiwakumbusha kufanya hivyo, vinginevyo hawatoweza kufanya usajili.

Yanga hivi karibuni, FIFA na TFF iliifungia kwa kutomlipa aliyekuwa mchezaji wake, Hafiz Konkoni raia wa Ghana ambaye alipewa mkono wa kwaheri katikati ya usajili wa msimu uliopita, baada ya kusajiliwa mwanzoni mwa msimu huo.

Hata hivyo, Yanga imewatoa hofu wanachama na mashabiki kuwa itatekeleza maagizo hayo.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe amesema klabu hiyo italipa madeni ya wachezaji wote wanaodai, hata wale ambao itawapa mkono wa kwaheri msimu huu.

## Saido asepa na mabao 24 Simba

INATOKA UKURASA 24

kumpata mwenye kiwango kizuri anayeendana na falsafa ya Simba na mazingira pia.

"Niwaambie tu wanachama na mashabiki wa Simba kila kitu kiko vizuri, kuanzia usajili hadi eneo la benchi la ufundi, nadhani hata mwekezaji wetu, Mohamed Dewji alilieleza hilo, msimu uliopita tulibezwa sana na kupewa kila aina ya manyanyaso na masimango hali iliyomtoa Ughaibuni mwekezaji wetu kuja kushika kijiti cha usajili kwa kuhakikisha hatufanyi makosa tena," alisema Ahmed.

Taarifa zinaeleza kuwa mkononi yalibaki majina ya makocha wanne ambayo ni Florent Ibenge raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo anayeifundisha Al Hilal ya Sudan, Mreno, Alexandre Santos anayemaliza mkataba wake na Klabu ya Petro de Luanda ya Angola, Omar Najhi, raia wa Uingereza mwenye asili ya Morocco, pamoja na anayetajwa kuwa na asilimia kubwa ya kupewa mikoba ya kukinoa kikosi hicho, Steve Komphela raia wa Afrika Kusini, anayeifundisha Klabu ya Lamontville Golden Arrows ya Sauzi.

Wakati akitangaza wajumbe wapya wa Bodi ya Wakurugenzi upande wake, Mo, alitaja sababu mbalimbali zilizoikwamisha Simba kufanya vema, ikiwamo kutokuwa na benchi zuri la ufundi akiahidi kulifanyia kazi.

"Tumeshindwa kutegeneza timu bora ya ushindani, eneo la benchi la ufundi halikuwa zuri, hii imesababisha hata kupoteza falsafa yetu ya pira-biriani, hili ni eneo muhimu la kufanyia kazi, naahidi tutashirikiana na wenzangu kusuka upya eneo hilo," alisema.

# PAMBA YAMTAMBULISHA RASMI KOPUNOVIC KUINOA

**Na Adam Fungamwango**

HATIMAYE Klabu ya Pamba FC imemtambulisha rasmi kocha wa zamani wa Simba na Tabora United, Goran Kopunovic, ambaye amepewa jukumu la kuinoa timu hiyo badala ya Mbwana Makata ambaye ameipandisha daraja.

Siku chache zilizopita, Nipashe liliandika taarifa za ndani za klabu hiyo kuwa kwenye mazungumzo na kocha huyo, sasa yamekamilika na kusaini mkataba wa mwaka mmoja.

**Taarifa iliyotolewa jana na klabu hiyo imeeleza baada ya mazungumzo ya muda mrefu, hatimaye amekubali kuifundisha klabu hiyo kwa kipindi hicho.**

"Rasmi, Goran amekubali azimio la miamba wa Pamba FC kwa kandarasi ya mwaka mmoja," ilisomeka sehemu ya taarifa hiyo.

Goran anachukua mikoba ya Makata ambaye aliipandisha timu hiyo mara ya kwanza baada ya miaka 23.

Pamba, iliyoshuka daraja 2001, ilipanda msimu huu, ikishika nafasi ya pili nyuma ya KenGold.

Goran anayependa soka la chini, pasi fupi fupi na kasi, aliifundisha Simba mwaka 2015 na kutwaa Kombe la Mapinduzi, Zanzibar mwaka huo.

Pamba iliwahi kutwaa ubingwa wa Jamhuri ya Muungano mwaka 1990, ikiwa na wachezaji mahiri wakati huo kina Khalid Bitebo 'Zembwela', Paul Rwechungura', Madata Lubigisa, Hamza Mponda, Kitwana Selemani, David Mwakalebela, Deo Mkuki, Alfonce Modest, George Masatu, Beya Simba, Fumo Felician, Nteze John, Hussein Masha, John Makelele 'Zig Zag', Khalfan Ngassa na wengineo, ikiivua Malindi ya Zanzibar, iliyokuwa bingwa mwaka 1989.

YALAAAH...



Leandro Trossard akilalama kuchezewa madhambi na mchezaji wa Slovakia katika mechi ya Kundi E ya michuano ya Euro iliyopigwa Uwanja wa Deutsche Bank Park, Ujerumani juzi usiku. Slovakia ilishinda bao 1-0. **PICHA: MTANDAO**

## *Biashara Utd yatamba kurudi na nguvu mpya*

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kushindwa kupanda Ligi Kuu Tanzania Bara kwa kufungwa jumla ya mabao 2-1 dhidi ya Tabora United katika mchezo wa mikondo miwili ya 'play off', Klabu ya Biashara United imekubali yaishe, ikiahidi itarudi na nguvu mpya msimu ujao.

Katika salamu zake za shukurani kwa wadau mbalimbali baada ya kumaliza msimu, Rais wa Klabu hiyo jana, Gabriel Rugumila alisema kila mmoja katika nafasi yake alifanya kazi nzuri, wakiwamo wachezaji na benchi la ufundi, lakini mwisho wa siku hawakupata kile walichokihitaji na wameumizwa mno, lakini akaahidi kurejea msimu ujao na nguvu mpya.

Katika mchezo wa kwanza uliopigwa Juni 2, mwaka huu, Uwanja wa Karume, Musoma mkoani Mara, Biashara United ilishinda bao 1-0, kabla ya kufungwa mbaao 2-0, Jumapili, Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi na kuzima ndoto zao za kutaka kurejea Ligi Kuu mara ya kwanza baada ya kushuka msimu wa 2021/22.

"Tumeipigania timu yetu mpaka jasho la mwisho, tunashukuru kumaliza msimu salama, tunalishukuru benchi la ufundi likiongozwa na Amani Josiah, Edna Lema na Ivo Mapunda ambao walifanya kazi nzuri, wakiwamo wachezaji wetu wote ambao wameitumikia timu kwa uaminifu mkubwa, lakini wameumizwa na matokeo ya mwisho na sisi pia tumeumia, ila matumaini yetu ni kujipanga kwa msimu ujao, tutarudi na nguvu mpya," alisema rais huyo.

Rugumila pia alimshukuru Mkuu wa Mkoa aliyeondoka, Said Mtanda ambaye kwa sasa amehamia Mwanza, pamoja na aliyekuwapo sasa kwenye mkoa wa Mara wa sasa, Venance Mtambi, wabunge na wafanyabiashara, pamoja na mashabiki kwa kujitolea kwao.

Baada ya kumaliza nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi ya Champinship, Biashara United iliifunga Mbeya Kwanza katika mchezo wa kwanza wa 'play off' jumla ya mabao 4-0, ikishinda 2-0 nyumbani na ugenini, kabla ya kukutana na kigingi, Tabora United.

# Michezo

Jumatano Juni 19, 2024

Nipashe




Celtics yaweka rekodi ubingwa UKURASA 22

ILIKUWA HIVI...




Mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe, akiruka kuwania mpira lakini akajikuta akilicheza kwa pua bega la beki wa kati wa Austria, Kevin Danso, kwenye mechi ya Kundi D ya michuano ya Euro 2024 iliyopigwa katika Uwanja wa Merkur Spiel-Arena, Ujerumani. Austria ilishinda bao 1-0. **HABARI UK, 21. PICHA: MTANDAO**

# MSUVA AFUNGUA MILANGO YANGA

**Na Adam Fungamwango**

## ●●● Fifa yaifungia kusajili huku ikiwatoa hofu wanachama wake kuwa...

WINGA wa Timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, Simon Msuva, amethibitisha kuwa amemaliza mkataba wake na Klabu ya Al Najma ya Saudi Arabia, hivyo kuzifungulia mlango Klabu za Yanga, Simba na Azam FC kumsajili kama zinahitaji huduma yake.

**Akizungumza juzi jijini Dar es Salaam, Msuva alisema mkataba wake na klabu hiyo ulikuwa ni wa msimu mmoja tu, hivyo sasa yupo huru kujiunga na klabu yoyote inayomhitaji, lakini aliwaambia mashabiki wake kutulia kwani chochote kitakachotokea atawaambia.**

"Mkataba kule nimemaliza chochote kitakachotokea nitawajulisha, sitaki kuongelea habari zozote kuhusu ofa kwa sasa, zipo nyingi ila muda ukifika nitawajulisha, kikubwa mashabiki wangu waelewe bado nipo Saudi Arabia, kuna timu nyingi kule za kuchezea, lakini pia kuna ofa kutoka sehemu mbalimbali Afrika, hivyo chochote kitakachotokea kipya basi Watanzania watakiona kwa upande wangu," alisema mchezaji huyo ambaye kabla ya timu hiyo alikuwa akiichezea JS Kablie ya Algeria.

Hivi karibuni Klabu za Simba na Yanga zimekuwa zikihusishwa kutaka kumsajili mchezaji huyo hasa kipindi hiki cha dirisha la usajili, ambaye mara ya mwisho kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara ilikuwa ni msimu wa 2017, akiwa na Klabu ya 'Wananchi.'

Msuva ambaye ni mmoja wa wachezaji wakongwe na tegemeo kwenye kikosi cha Stars, alianza karia yake ya soka katika kikosi cha Azam FC, 2010 hadi 2011, kabla ya kutimkia Moro United ambapo alicheza msimu mmoja, 2011 hadi 2012 na kutua Yanga, alipoichezea hadi 2017.

Mchezaji huyo alianza safari yake ya soka la kulipwa 2017 alipojiunga na Diffa el Jadida ya Morocco, hadi 2020 alipotimkia Wydad Casablanca ya huko, 2022 hadi 2023 akaichezea Klabu ya Al Qadsiah ya Saudia Arabia, baadaye JS Kablie na Al Najma.

Hata hivyo, wakati dirisha la usajili likiwa limefunguliwa usiku wa kumkia Jumamosi, Klabu za Yanga, Singida Fountain Gate, Tabora United, Biashara United na FGA Talents zimezuia kusajili mpaka pale zitakapowalipa wachezaji wanaozidai.

Taarifa iliyotolewa jana na Shirikisho la Mpira wa Miguu (TFF), ikisainiwa wa Ofisa Habari na Mawasiliano wake, Cliford Ndimbo, imesema kuwa klabu hizo zimefungiwa kwa pamoja na Shirikisho la Kimataifa la Mpira wa Miguu (FIFA), na TFF, hivyo haziwezi kuingiza mchezaji yoyote kwenye mfumo wa usajili wa kimataifa

"Klabu ambayo itawalipa wahusika, itaondolewa mara moja

INAENDELEA UKURASA 23

## Saido asepa na mabao 24 Simba

**Adam Fungamwango na Shufaa Lyimo**

KLABU ya Simba imeachana na kiungo mshambuliaji wake tegemeo, Saido Ntibazonkiza, baada ya kuhudumu kwa msimu mmoja na nusu, akipachika jumla ya mabao 24 katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Taarifa iliyotolewa jana na uongozi wa kabu hiyo, imeeleza haitaendelea tena na raia huyo wa Burundi, aliyesajiliwa kipindi cha dirisha dogo la uhamisho msimu wa 2022/23, akitokea Geita Gold.

"Uongozi wa klabu unawatangazia kuwa hatutaendelea kuwa na mchezaji Saido, baada ya mkataba wake kumalizika," ilisema taarifa hiyo.

Mchezaji huyo anaondoka Simba akiwa amefunga jumla ya mabao 24 katika misimu miwili ya Ligi Kuu Tanzania Bara, mabao 13 msimu wa 2022/23, na msimu uliomalizika akifunga 11.

Alimaliza akiwa kinara wa ufungaji msimu wa 2022/23, akiwa na mabao 17, sawa na straika Fiston Mayele wa Yanga, manne akitoka nayo Geita Gold na kuwa mchezaji aliyeongoza kuwa na mabao mengi katika kikosi hicho.

Msimu uliomalizika pia aliweka rekodi hiyo, kwani mabao 11 aliyopachika yalikuwa ni mengi zaidi ya mchezaji yeyote wa timu hiyo, akifuatiwa na Jean Baleke ambaye aliachwa kipindi cha dirisha dogo akiwa ameshapachika mabao manane.

Kabla ya kwenda Geita Gold, Saido, ambaye pia ni mchezaji wa Timu ya Taifa ya Burundi, aliichezea Yanga kuanzia 2020 hadi 2022.

Wakati Simba ikiachana na Saido, Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, amewatoa wasiwasi wanachama na mashabiki wa Simba kuhusu suala ya kocha.

Alisema suala hilo lipo chini ya kamati maalum kwa ajili ya kufanyiwa kazi ikiwa ni pamoja na kuchujwa kwa majina, ili

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >